# Nipashe

Alhamisi Juni 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580971

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



**SAKA HANA HARAKA NA MKATABA ARSENAL**

UKURASA 22

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,004,055,092/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Mahakama** yaagiza kukamatwa aliyebaka mama na mdhamini wake baba mzazi

UKURASA 4




# Utapeli wa upatu wawaliza wengi

• **Umedumu** tangu Machi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**MAAMBUKIZO MAPYA YA UVIKO-19 YAONGEZEKA**
WIZARA ya Afya imesema idadi ya maambukizo mapya ya ugonjwa wa UVIKO-19 imeongezeka na kufikia 161 ikilinganishwa na...

UKURASA WA 4
**TASAC YAONYESHA FURSA AJIRA UBAHARIA**
SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limetoa rai kwa wanafunzi kusomea taaluma ya ubaharia ili...

UKURASA WA 7
**MWALIMU MAZOEZI MBARONI AKIDAIWA KUNAJISI MWANAFUNZI**
ALIYEKUWA mwalimu wa mazoezi katika Shule ya Msingi Mkombozi, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Abel Bulugwe (21)...

## Majaliwa atoa siku 5 pikipiki zifike kwa maofisa ugani

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua pikipiki zilizoko katika Ofisi za Wizara ya Kilimo, jijini Dodoma jana, ambazo zilitolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya maofisa ugani nchini kote. Kushoto ni Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde. **PICHA: OWM**



## Samia: Ahueni zaidi bei ya petroli inakuja

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAWABAKISHA MZAMIRU, ONYANGO UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Utapeli wa upatu wawaliza wengi

**Na Romana Mallya**

UTAPELI wa aina yake katika upatu umewaliza Watanzania wengi ambao walijiunga na kuwekeza kwenye programu maarufu mtandaoni ijulikanayo kama Idea Debater kwa lengo la kuvuna fedha lakini wakajikuta wakipigwa fedha zao kwa kuwa programu hiyo imefungwa.

Ilikuaje? Mwezi Machi mwaka huu, programu hiyo iliyowaunganisha mamia kwenye makundi ya WhatsApp, ilipata umaarufu wa ghafla baada ya Watanzania wengi kujiunga nayo, wakihamasishana kuwekeza fedha zao ili wawe wanavuna faida kila siku.

Ili kujiunga na programu hiyo, mhusika aliunganishwa kwenye makundi ya WhatsApp kisha kufuata maelekezo ya namna ya kuingia na kujaza taarifa muhimu zinazohitajika na baada ya hapo aliweka fedha kulingana na uwezo wake.

Lyimo (jina la pili tunalihifadhi), mkazi wa Dar es Salaam, ni miongoni mwa walioweka na kulizwa, anasimulia kuwa Idea Debater kwa mujibu wa taarifa alizopokea kwenye WhatsApp baada ya kutumiwa, ni jukwaa lililozinduliwa Tanzania mwezi Machi mwaka huu na lilitengenezwa na ABE.

Kwa mujibu wa taarifa hizo alizopokea, kampuni kama Amazon, eBay, shopee na Lazada hufanya biashara za bidhaa mbalimbali na hata kujitangaza mtandaoni ili kutafuta na kuwavuna wateja wengi zaidi.

Alisema ili upate faida ya kamisheni ya kila siku ya asilimia tano hadi nane kwa kukamilisha kazi 20 za kuweka oda kila siku, mtu alitakiwa kuweka salio katika akaunti na ilipofika saa 8:00 usiku, oda mpya zilikuwa zikiwekwa.

Alisema kiwango cha kwanza (ngazi ya chini) cha kuwekeza kilikuwa kiingilio cha Sh. 10,000 na cha juu Sh. 199,999 na faida yake ni asilimia tano ambapo mtu hupata 500 kwa siku ikiwa ataweka fedha hiyo.

Lyimo alisema aliweka Sh. 100,000 ikiwa ni hatua ya awali ili avune asilimia tano lakini programu hiyo ikafungwa na anachokishuhuia sasa ni kuona fedha kwenye akaunti ya programu hiyo, lakini hawezi kutoa.

"Hii ilikuwa mara yangu ya kwanza kuwekeza hivyo, niliweka fedha hii ili niweze kuvuna zaidi," alilalamika na kubainisha kuwa waendeshaji wasiojulikana wa programu hiyo waliwaunganisha wateja kwenye kundi la WhatsApp.

"Ni makundi ambayo ninaamini yalivutia watu wengi ndani ya muda mfupi kwa sababu kulikuwa na watu walikuwa wakiuliza maswali ya mara kwa mara kwa viongozi kuhusiana na programu hii," aliongeza.

Mwathirika mwingine wa utapeli huo, Jackson (jina la pili tunalihifadhi), alisema kwa mara ya kwanza wakati anajiunga, aliamini ipo siku angetapeliwa fedha zake lakini hakujua ni lini.

"Unapotoa kiwango kikubwa cha fedha mfano Sh. 300,000 au Sh. 500,000 ilikuwa inachukua muda kupokea, unaulizwa maswali 'umeleta wawekezaji wangapi?' ukithibitisha ndipo utapatiwa.

"Nilijua ipo siku ingefikia hatua hii iliyopo sasa lakini sikuwa na uhakika ni lini. Kwa hiyo, nilikuwa nawekeza kwa tahadhari na kutoa ndani ya muda mfupi na uwekezaji mkubwa niliofanya kwenye programu hii ni Sh. 200,000," alisimulia.

Alisema jambo lililomtia shaka ni waendeshaji wa programu wakati wa kuweka fedha wanatumia akaunti moja lakini wakati wa kuvuna (mteja) alitumiwa kupitia mawakala tofauti.

**KAULI YA SERIKALI**

Akizungumzia suala hilo, Msemaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, alisema wizara hiyo haifahamu programu hiyo na kuwaonya Watanzania dhidi ya kujiunga nayo.

Mwaipaja alisema inasikitisha kwamba watu hawa wametapeliwa fedha zao na kwamba hilo ni tukio la uhalifu kama matukio mengine ya uhalifu.

Alisema Serikali ilishapiga marufuku masuala ya upatu na mengine yanayoshabihiana na aina hiyo lakini bado yanaendelea kutokea.

Mwaipaja aliwataka wanaotaka kuwekeza, kupeleka fedha na mitaji yao katika taasisi zinazotambuliwa kisheria, yakiwamo masoko ya hisa.

Kwa mujibu wa programu hiyo, kwa ngazi ya pili, kiasi cha chini cha kuingia ni Sh. 200,000 na juu ni Sh. 499,999 na faida ni asilimia sita kwa siku ambayo ni Sh. 12,000.

Ngazi ya tatu inaanzia Sh. 500,000 na kiwango cha juu kwa kundi hilo ni Sh. 1,999,999 na faida ni asilimia saba ya kiasi kilichowekwa, ikimaanisha 35,000 kwa siku kama mtu ataweka Sh. 500,000.

Ushawishi mwingine kwa waliokuwa wanajiunga na programu ni kwa watumiaji wapya ambao Idea Debater iliahidi kuwawezesha kupata zawadi ya Sh. 2,000 kila mwekezaji anapomwalika mteja mpya na mara tu atakapolipia, atapata Sh. 1,000.

Ada ya kutoa fedha ndani ya programu hiyo ilikuwa asilimia nne na kutoa kwa njia nyingine waliyoiita USDT walihitaji 1USDT kama ada ya usindikaji bila kujali kiasi mteja atakachotoa. Sasa programu hiyo imefungwa kwa wanaohitaji kutoa fedha zao.



Muuguzi wa Afya wa Hospitali ya Tumbi Kibaha mkoani Pwani, Doreen Richard (katikati), akiwapima wananchi waliofika hospitalini hapo jana, kwa ajili ya huduma ya kupima magonjwa mbalimbali bure, iliyofadhiliwa na Taasisi ya Al- ATA 'A Charitable (ACF) Tanzania, chini ya Shirika la Misaada la Kimataifa la Qatar Charity. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia: Ahueni zaidi bei ya petroli inakuja

**Na Richard Makore,** BUKOBA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kuendelea kutoa ruzuku ya fedha kwa kila mwezi, ili kusaidia kupunguza bei ya mafuta ya dizeli na petroli iliyopanda nchini.

Alitoa ahadi hiyo jana katika eneo la Bwanga wilayani Chato mkoani Geita akiwa njiani kuelekea mkoani Kagera kwa ajili ya ziara ya siku tatu.

Rais alisema kupanda kwa bei ya mafuta ni janga la dunia nzima kutokana na vita vya Urusi na Ukraine vinavyoendelea na kwamba serikali anayoiongoza haijasababisha hali hiyo.

Alisema dunia nzima inalia kutokana na vita hivyo na nchi kubwa zinapopigana madhara ya moja kwa moja huzipata nchi nyingi.

"Bei ya mafuta imepanda sana, ni dunia nzima na siyo kwa Tanzania pekee na serikali inafanya jitihada kuhakikisha inashuka kwa kuendelea kutoa ruzuku kila mwezi," alisema.

Mwezi huu serikali imetoa ruzuku ya Sh. bilioni 100 ili kupunguza bei ya mafuta ya dizeli na petroli nchini.

Akizungumza na wananchi waliompokea eneo hilo, Rais Samia aliwataka kuendelea kuwa wavumilivu kwa kuwa serikali inafanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuendelea kutoa ruzuku mpaka hapo bei itakapokaa sawa.

Kuhusu uhaba wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa Bwanga, Rais Samia aliwataka kupunguza mifugo ili wawe na mifugo michache inayofungwa kisasa kwa kutumia eneo dogo.

Alisema idadi ya watu inazidi kuongezeka kutokana na jamii kuzaliana kwa kasi, akisisitiza kuwa hiyo ni moja ya vyanzo vya ardhi kuonekana haikidhi mahitaji.

Mbunge wa Chato, Dk. Medadi Kalemani, alimshukuru Rais Samia kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo huku akimwomba kulipatia ufumbuzi suala la uhaba wa ardhi unaowakabili wananchi wake.

Rais Samia pia aliagiza fedha zote za miradi kusimamiwa vizuri Ili zipeleke maendeleo kwa wananchi.

Akiwa wilayani Biharamulo, Rais alisema fedha nyingi zinapelekwa kwa wananchi na kuahidi kwamba kila wanapokusanya mapato, wahakikishe wanayapeleka kwenye maendeleo.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema wamejiandaa kwa s ensa ya watu na makazi iliyopangwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu.

Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamadi Masauni, aliahidi kumaliza tatizo la upatikanaji wa vitambulisho vya taifa huku Mbunge wa Kyerwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akimshukuru Rais kwa kusaidia bei ya kahawa kupanda.

# Maambukizo mapya ya UVIKO-19 yaongezeka

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Afya imesema idadi ya maambukizo mapya ya ugonjwa wa UVIKO-19 imeongezeka na kufikia 161 kulinganishwa na 68 yaliyotokea Aprili 2 hadi Mei 4 mwaka huu.

Taarifa iliyotolea juzi na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, ililitaja ongezeko hilo kuwa ni sawa na asilimia 137.

Alisema idadi ya waliothibitika kuwa na ugonjwa huo katika kipindi cha Mei 5 mwaka huu hadi Juni 3 mwaka huu inaonyesha kuwa Dar es Salaam viliripotiwa visa 130, Arusha (10), Mwanza (5), Shinyanga (4), Mtwara (3), Dodoma (2), Mara (2), Morogoro (1), Simiyu (1), Katavi (1), Kilimanjaro (1) na Mbeya (1).

Alisema wagonjwa watatu waliothibitika kuwa na UVIKO-19 walilazwa na wote walikuwa hawajapata chanjo.

Alisema hali hiyo inaashiria maambukizo yameanza kuongezeka kwa jamii lakini katika kipindi cha miezi miwili mfululizo hakuna kifo kilichoripotiwa.

Mganga Mkuu wa Serikali alisema takwimu zilizotolewa zinaonyesha chanjo ni kinga dhidi ya madhara yatokanayo na UVIKO-19 na Serikali inaendelea kuitoa ili wananchi waendelee kuipata.

Mtaalamu huyo alibainisha kuwa kuanzia Mei 5 mwaka huu hadi Juni 3 mwaka huu, wananchi waliopata dozi kamili ya chanjo ni 775,680.

Tanzania iliripotiwa kupata mgonjwa wa kwanza wa UVIKO-19 Machi 16, 2020. Ugonjwa huo uligundulika kwa mara ya kwanza Wuhan, China Novemba 2019.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa aipa siku tano wizara kusambaza pikipiki

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa siku tano kuanzia jana hadi Juni 12 Wizara ya Kilimo iwe imeondoa pikipiki zote wizarani huko na kuzikabidhi kwa wakurugenzi.

"Hii haikubaliki, wakurugenzi wote waandikiwe barua waje wazichukue, kama kuna ufungaji wa 'plate number' utafanyika huko huko. Jumapili saa 10 jioni ziwe zimefika kwa wahusika," aliagiza.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana jijini hapo alipokagua ofisi za Wizara ya Kilimo zilizoko eneo la VETA, Dodoma na kukuta pikipiki zilizotolewa kwa ajili ya maofisa ugani zikiendelea kuwapo wizarani huko.

Aprili 4, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua ugawaji wa vitendea kazi vilivyoandaliwa na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya maofisa ugani wote nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na pikipiki.

Majaliwa alisema tayari Rais Samia alishazikabidhi kwa ajili ya kupelekwa kwa maofisa ugani, hivyo kitendo cha pikipiki hizo kuendelea kubaki katika eneo hilo hakikubaliki.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Profesa Siza Tumbo, alimhakikishia Waziri Mkuu kwamba wamepokea maelezo hayo na watayafanyia kazi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema (wapili kulia), akiwa na wafanyakazi wa Barrick Bulyanhulu, baada ya kuwakabidhi cheti cha shukrani kwa niaba ya kampuni hiyo, na kuunga mkono Tamasha la Utamaduni, lililomalizika mkoani humo jana. Kushoto ni Kaimu Meneja wa Uhusiano na Mazingira wa Barrick Bulyanhulu, Zuwena Senkondo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DPP atoa kibali kesi ya uhujumu isikilizwe Kisutu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imesikiliza kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Masoud Said na wenzake watano wanaotuhumiwa kukutwa na nyara za serikali na silaha baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kuwasilisha kibali cha kuruhusu mahakama hiyo kusikiliza.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mohamed Aminu, Seph Mwange, Fikiri Yusouph, Juma Said na Jumanne Mohamed.

Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, kuwa upelelezi umekamilika, hivyo aliwasilisha mahakamani kibali cha DPP kuruhusu mahakama hiyo kusikiliza shauri hilo pamoja na kuwasomea upya washtakiwa mashtaka yao na maelezo ya awali.

Akisoma hoja hizo, Wakili Mzava pamoja na mambo mengine, alidai washtakiwa wote kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali, kumiliki silaha na risasi.

Wakili Mzava alidai kuwa Machi 19, 2018 polisi walipata taarifa iliyosaidia kukamatwa kwa mshtakiwa Said huko Mbagala, Dar es Salaam ambaye alikubali kuhusika na uuzaji wa nyara za serikali, kumiliki silaha na kuwataja washtakiwa wenzake.

Alidai kuwa Machi 21, 2018, Said aliwapeleka polisi Kijiji cha Nyamwili kilichoko Rufiji mkoani Pwani ambako alikamatwa mshtakiwa Yusouph nyumbani kwake na katika upekuzi alikutwa na silaha.

Alidai kwamba Machi 22, 2018, mshtakiwa Aminu na Mwange walikamatwa Kijiji cha Nyamwili katika eneo ambalo walipanga kwenda kukutana na mteja ili kuuza nyara za serikali.

Wakili Mzava alidai washtakiwa hao walipokamatwa walikutwa na vipande 11 vya ngozi ya mamba na fuvu la kifaru.

Alidai kuwa baadaye mshtakiwa Aminu aliwapeleka polisi nyumbani kwake ambapo alikutwa na silaha aina ya shortgan yenye risasi 66 na maganda 38, lita 12.5 za mafuta ya kiboko, pakti 19 za chumvi na kujazwa katika fomu ya upekuzi.

Baada ya kusomwa hoja hizo, washtakiwa walikana tuhuma hizo isipokuwa majina yao na kwamba kweli wanakabiliwa na kesi hiyo.

Kesi hiyo imepangwa kusikilizwa Juni 22, mwaka huu, ambapo upande wa mashtaka utaanza kuleta mashahidi wake.

IITA Transforming African Agriculture 50 1967-2017

## POSITION ANNOUNCEMENT

## ACCOUNTS CLERK

## IITA-TZ-2022-ADM-007-NRS-DSM

**Background:** The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) invites applications for the position of an **Accounts Clerk.**

**The International Institute of Tropical Agriculture (IITA)** is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit https://www.iita.org/ for more information on IITA.

**Duty Station:** The position will be based at the IITA Regional Hub for Eastern Africa in Dar es Salaam, Tanzania.

**Qualifications:**

- Diploma in Accounting with at least 2 years' proven accounting experience
- Competency in MS Office, databases and accounting software
- Familiarity with booking keeping and basic accounting procedures
- Accuracy and attention to detail
- Ability to perform filing and record keeping tasks
- Previous experience in an NGO will be an added advantage
- Ability to manage multiple tasks at the same time in a demanding work environment
- Experience working a multicultural environment with good interpersonal skills
- Written and oral proficiency in English is required including mastery of English grammar and spelling, punctuation, paragraph and sentence structure.

**Responsibilities:**

- Record and reconcile cash advances to assure retirements of advances are done on time.
- Monitor and control the cash advance system
- Attend to various accounting queries.
- File and maintain financial support documents in hard copies
- Retrieve files as required from the archives.
- Liaise with the pension security fund offices on the reconciliation of monthly Pension remittances.
- Assist in the reconciliation of the IITA staff welfare records.
- Any other duties as assigned by supervisor

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Morogoro. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to
**IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# Mahakama yatoa hati kukamatwa anayedaiwa kumbaka mama yake

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Iringa imetoa hati ya kukamatwa kwa mfanyabiashara Kaloli Mkusa (30) pamoja na baba yake mzazi ambaye alimwekea dhamana, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 pamoja na kulipa fidia ya Sh. milioni moja kwa kosa la kumbaka mama yake mzazi.

Mfanyabiashara Kaloli Mkusa mwenye umri wa miaka 30 na mkazi wa Kijiji cha Msisina wilayani Iringa mkoani Iringa hakuwapo mahakamani wakati hukumu inatolewa.

Mtuhumiwa wa ubakaji na baba yake, Joseph Mkusa, aliyemwekea dhamana katika kesi hiyo, wanadaiwa kumetoweka kijijini huko na kwenda kusikojulikana.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Emmy Nsangalufu, amesema mtuhumiwa alifanya tukio hilo Mei 7, mwaka jana.

Alisema kuwa mtuhumiwa Kaloli Mkusa alikuwa akifanya biashara zake Tunduma mkoani Songwe na alirudi nyumbani na kufikia kwa baba yake ambaye anaishi nyumba tofauti na mama yake kutokana na kutalakiana.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa siku ya tukio, mtuhumiwa alikwenda nyumbani kwa mama yake majira ya usiku na kuvunja mlango huku akiwa ameshika panga na kumtisha kumkata kwa kumpiga kwa ubapa wa panga.

"Licha ya mama yake kumsihi asifanye hivyo, mtuhumiwa aliendelea na tukio hilo mpaka alipotimiza haja yake," hakimu alisema wakati wa kutoa hukumu.

Ilidaiwa kuwa baada ya tukio hilo, mama mzazi alitoa taarifa kwa majirani na baadaye Serikali ya Kijiji ndipo taratibu za kumkamata zikafanyika. Kesi hiyo iliendeshwa na Wakili wa Serikali, Jackline Nungu pamoja Alice Thomas, ikihusisha na imani za kishirikiana.

Kwa mujibu wa mahakama, kifungo hicho kitaanza kutumika pindi mtuhumiwa atakapokamatwa.



Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Edwin Iwato (kulia), akimwelimisha mlipakodi wa Mji wa Kahama, kuhusu masuala mbalimbali ya kodi wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea mkoani Shinyanga jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# TASAC yaonyesha fursa ajira ubaharia

**Na Elizabeth Zaya,** BAGAMOYO

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limetoa rai kwa wanafunzi kusomea taaluma ya ubaharia ili iwasaidie kuondokana na tatizo la ajira.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usalama na Ulinzi wa Vyombo vya Usafiri Majini na Utunzaji wa Mazingira wa TASAC, Baharia Gabriel Manase, alitoa rai hiyo jana mjini hapa alipowasilisha mada kwenye semina ya wahariri na waandishi wa habari.

Alisema sekta ya ubaharia kwa sasa ina fursa kubwa ya ajira tofauti na watu wanavyodhani.

"Vijana wengi wanaona sekta hii ya ubaharia ni ya kihuni, ninataka niwaambie kwamba kati ya sekta zenye fursa kubwa ya ajira ni pamoja na hii na ina wasomi wazuri sana.

"Mwaka jana kuna fursa kubwa ilipatikana ya kupeleka mabaharia kwenda kufanya kazi nje ya nchi. Kwa hiyo, walikwenda.

"Na mpaka sasa bado mabaharia wanahitajika kwa wingi. Kwa hiyo, niwaombe vijana na wanafunzi wasomee hii sekta ina fursa kubwa. Kipindi cha COVID-19, mahabaria zaidi ya 400 walikuwa wanahitajika kwenda kufanya kazi nje ya nchi," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa miaka ya nyuma, sekta hiyo ilikuwa inaonekana si nzuri kusomea na hivyo ni vyema vijana na wanafunzi wakabadilisha mawazo yao na kwenda kusomea ili waondokane na tatizo la kukosa ajira.

Manase alisema bado lipo hitaji kubwa katika sekta hiyo hususani kwa mabaharia katika meli za kimataifa na hivyo kusisitiza vijana kujitokeza zaidi kusoma fani hiyo yenye ajira nyingi duniani.

Alisema zipo kampuni nyingi za ndani na nje ya nchi ambazo zimekuwa zikihitaji mabaharia kwa ajili ya kufanya nao kazi.

# Wabunge wataka wahitimu wakopeshwe kwa vyeti vyao

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imesema inaangalia uwezekano wa kutumia vyeti vya wahitimu wa vyuo vikuu nchini kama dhamana ya kuwapa mikopo mbalimbali ya kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wengine.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, akibainisha kuwa serikali ina mifuko zaidi ya 45 inayohusika na mikopo mbali na mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri inayotolewa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Latifa Juakali, alitaka kujua mpango wa Serikali kuanzisha bodi ya mitaji kwa wahitimu wa elimu ya juu kama ilivyo kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Akijibu swali la msingi, Naibu Waziri alisema Serikali imeupokea ushauri wa mbunge na kwamba imekuwa ikitoa mikopo kwa vijana kupitia halmashauri kwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani, huku akiwashauri wahitimu hao kutumia fursa hiyo kupata mitaji.

"Tunaangalia namna gani wahitimu watatumia vyeti vyao kupata mikopo tutaifanya tathmini na kufanya uamuzi, hili ni jambo mtambuka, linahusu wizara nyingine. Tunachukua ushauri ili tuone kama vyeti vinaweza kutumika kamdhamini mhitimu," alisema.

Naibu Waziri Kipanga pia alisema halmashauri zinatenga asilimi 10 ya mapato ya ndani ya kwa ajili ya kutoa mikopo kwa mgawanyo wa asilimia nne vijana, asilimia nne wanawake na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu.

"Mwanzoni ilikuwa lazima vijana 10 wawe kwenye kikundi na wawe na shughuli ya kufanya, kwa sasa masharti yamelegezwa hata wakiwa watano katika kikundi wanapewa mikopo ya kukidhi mahitaji yao ili waweze kurejesha na kujiajiri," alifanua.

Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya, alihoji ni lini wizara hiyo itatenga fungu maalum kusaidia vijana kama wanavyotoa mikopo ya elimu ya juu, huku akitolea mfano wa Wizara ya Kilimo inayotoa motisha kwa vijana wanaojiunga na kufanya shughuli za kilimo mara baada ya kuhitimu masomo yao.

Akijibu swali hilo, Waziri Kipanga alisema jukumu la wizara ni kuratibu utoaji wa elimu nchini na wakishahitimu siyo jukumu lao pekee, bali la Serikali kwa ujumla, lakini kwa kuwa mbunge huyo anazungumzia motisha ili wajiajiri, Serikali inapokea ushauri huo.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritha Kabati, alitaka kauli ya serikali kuhusu wahitimu wa vyuo vikuu kukatwa fedha zaidi licha ya kumaliza mikopo yao.

Waziri Kapinga alisema bodi imeanzisha dawati la malalamiko na kuwataka wahitimu walioendelea kukatwa fedha kupeleka hoja zao na itakapobainika walikatwa kimakosa watarejeshewa fedha zao.

Alisema mfumo wa mikopo hiyo unaonyesha nani kakopeshwa, karejesha kiasi gani na kimebaki kiasi gani, jambo linalowawezesha wanufaika kuona mwenendo wa deni lao.



## MAPINDUZI YA BIMA KWA WOTE

# Sababu za NMB Bank kuongoza huduma za bima

***Na Costantine Muganyizi***

Bila ubishi, bima jumuishi kama namna nyingine za kujiwekea fedha, ina umuhimu mkubwa katika usalama wa kifedha wa mtu binafsi na ustawi wa mataifa.

Hata hivyo, nchini Tanzania huduma ya udhibiti wa hatari ume¬chukua muda kuchangia katika kuboresha maisha kwa wote.

Miongoni mwa sababu zilizoche¬lewesha huduma za bima kufanya vizuri imekuwa ni kutokuwepo kwa chaneli za kibinifu za usambazaji kama bancassurance, bima inayo¬tolewa na kampuni za bima kwa kutumia huduma za kibenki.

Tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo kisheria karibu miaka mita¬tu iliyopita, mpango huo ambao huwezesha benki kuuza huduma za bima kama wakala wa mashirika ya bima, imekuwa na mafanikio makubwa huku NMB Bank ikifanya maajabu katika soko.

**Huduma ya bima kwa NMB**

Katika mahojiano ya hivi kari¬buni, mtaalamu wa bima wa benki hiyo, Martine Massawe, alisema NMB Bancassurance inafanya vizuri sokoni kwa sababu ya unafuu wa vifurushi vyake, utatuzi wa kibu¬nifu na upatikanaji wake usio na matatizo.

Pia, Massawe alisema huduma ya bima inapatikana sawasawa nchi¬ni, na kwamba inakwamishwa kwa kiasi kikubwa na hali ya wananchi kutokuwa na ufahamu, huku walio mikoani ndio wakiathirika zaidi.

Benki hiyo ilikuwa ya kwanza kupewa leseni ya kutoa huduma za bima mwaka 2020 na tangu wakati huo imekuwa ikiongoza katika kila kitu kinachohusu bancassurance.

Licha ya kuuzika sana kwa vifu¬rushi vilivyo na ubunifu vya bima, NMB ina mkakati wa kushughulikia matatizo ya uendeshaji ambayo yamekwamisha nafanikio ya sekta hiyo.

UMEBIMA? – Si Ngumu Kihivyo

**Hivyo ndivyo mpango kama wa bima ya UMEBIMA wa kuelimisha kuhusu bima ulivyozaliwa. Kitu cha kwan¬za kilichofanywa na NMB chini ya mpango huo wa elimu na kuhama¬sisha umma kilikuwa ni kutambuli¬sha huduma kwa umma kwa kuuliza swali – Umekata bima?**

Baadaye viongozi wa kampeni hiyo walionyesha na kuelezea kuwa si vigumu kwa mtu kujilinda kwa bima kama inavyochukuliwa kima¬kosa. Na wakaongeza kuwa suala hilo ni rahisi kama ABC wakati mtu anapohitaji na kupata bima kwa kutumia huduma ya NMB Bancas¬surance.

Akizungumza katika hafla ya kuz¬indua raundi ya pili ya kampeni za UMEBIMA mwezi Februari, mkuu wa huduma za benki kwa wateja na biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema kimsingi kampeni inalenga kuelimisha umma faida za kuweka bima ya maisha na mali na ni kwa jinsi gani inaweza kufanyika kirahisi kwa kutumia huduma za bima za benki hiyo.

Mponzi alisema kampeni ya uhamasishaji kuhusu bima imekuwa kitu kingine cha mabadiliko amba-cho NMB imekifanya kuendeleza bima kwa kutumia huduma za benki na kuchangia kufikia malengo ya taifa ya ujumuishaji katika huduma za bima.

"Kutojua manufaa ya bima si tu kulipunguza kulifinyisha matumizi ya huduma za bima, bali pia kuli-changia kwa kiasi kikubwa kutokua kwa sekta na kupunguza mchango wake katika Pato la Taifa (GDP)," Massawe aliliambia gazeti la Nipashe katika mahojiano hayo.

**Utatuzi wa kibunifu na vifurushi**

"Hata hivyo, hilo ni suala la kihis¬toria kwa kuwa miaka miwili ya ban¬cassurance, haijaongeza matumizi ya bima na kusaidia kubuni utatuzi mpya pekee, bali pia limechangia kwa kiasi kikubwa katika kuelimi¬sha watu kuhusu huduma hiyo na manufaa yake makubwa," alisema.

Massawe alisema mafanikio ya bancassurance ya NMB hayakami¬liki bila ya kutaka utatuzi tofauti wa kibunifu ambao unatokana na benki hiyo kushirikiana na mashirika ya bima kuzindua huma hiyo sokoni.

Orodha hiyo inajumuisha vifu¬rushi kama Group Funeral Cover (GFC) au vikundi vya kushikana mkono wakati wa mmisiba, Ushiri¬ka Afya, Fanaka, na Jahazi kwa ajili ya wadau katika uvuvi na kifurushi kilichozinduliwa hivi karibuni cha wafanyabiashara wadogo kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya moto cha Machinga Fire Insurance.

**Bima ya machinga dhidi ya moto na misiba**

Bidhaa hii imebuniwa kwa ajili ya wamiliki wa niashara ndogondogo dhidi ya athari za moto na mafuriko na ambayo pia imeongezewa kubi¬ma hadi ulemavu wa kudumu wa mmiliki wa biashara.

Kiwango kinacholipwa kwa bima hii ni kati ya Sh10,000 na Sh60,000, wakati malipo kwa mnufaika yanakuwa kati ya Sh500,000 na Sh10 milioni kutegemea na kanuni za kifurushi kilichonunuliwa.

Kifurushi cha bima ya pamoja (Group Insurance Policy) kwa makundi rasmi na yasiyo rasmi kama ya WhatsApp, Vicoba), koo au familia ni mpango unaotokana na ushirikiano na shirika la Metro¬politan Life.

Massawe alisema wakati mwa¬nakikundi amefariki, bima hiyo mpya hulipia gharama za mazishi na faida zake zinaweza kwenda hadi kwa familia ya mwanakikundi ali¬yekuwa na bima hiyo hali kadhalika wazazi na wakwe. Huduma hiyo pia inamnufaisha mwanakikundi ali¬yepata ulemavu wa kudumu.

**Ushirika Afya, Jahazi na Fanaka**

Mpango wa Bima ya Ushirika Afya ni ushirikiano na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa ajili ya kuwawezesha makulima mahitaji ya huduma za afya kwa kuwapa miko¬po isiyo na riba ya NMB ambayo hulipa baada ya kuuza mazao yao mwishoni mwa msimu wa kilimo.

Kifurushi cha bima cha Jahazi Insurance kilibuniwa kwa ushiriki¬ano na shirika la bima la Britam kwa ajili ya sekta ya uvuvi. Huduma hiyo inalenga biashara za uvuvi na imebuniwa kuwalinda wavuvi dhidi ya moto, wizi, kuzama pamoja na madeni ya wadau wengine.

> **2020**
>
> **Benki hiyo ilikuwa ya kwanza kupewa leseni ya kutoa huduma za bima mwaka 2020 na tangu wakati huo imekuwa ikiongoza katika kila kitu kina chohusu bancassurance.**

Desemba 2021, NMB na shirika la bima la Jubilee Life Insurance wal¬izindua mpango wa Fanaka kuwa¬vutia wateja kutoka daraja la kati na jumuisha ya wafanyabiashara.

Huduma hiyo inashughulikia bima ya maisha ya walioinunua wakati ikimpa pia fursa ya kuwekeza kidogo kidogo katika kipindi Fulani na kuzipata kwa mkupuo kulingana na kanuni za huduma hiyo muda unapofika.




*Filbert Mponzi, mkuu wa huduma za rejareja za benki na biashara wa NMB (kushoto), akinyanyua UMEBIMA? – bango la kampeni ya SINgumuKihivyo—kuzindua rasmi mpango wa mwaka huu wa elimu ya bima kwa ajili ya kuelimisha wananchi manufaa ya kuweka bima ya maisha na mali katika soko la Karume, Ilaya jijini Dar es Salaam Machi 7, 2022. Anayemsaidia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Life, Hellen Mzela na wa pili kushoto ni manaja wa NMB, kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard.*

Kifurushi cha Fanaka pia kinatoa mwendelezo wa bima ya maisha hadi miaka 90 kwa aliyekata, licha ya kutokuwa na miaka ya ziada.

"Unafuu, upatikanaji na urahisi ni muhimu sana katika masoko ya nchi maskini kama yetu na hapo ndipo sisi tunafanya vizuri – kubuni na kuendeleza utatuzi mpya na vifu¬rushi vya kibunifu kwa ajili ya kuki¬dhi mahitaji maalum kwa ajili ya masoko tofauti," alisema Massawe.



> **Nachukua na¬fasi hii kuishuk¬uru Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) kwa kuziruhusu ben¬kki kushiriki ka¬tika biashara ya kutoa huduma za bima kwa sababu hii itaongeza ushindani na ubunifu katika sekta. Tutahakikisha kuwa kila mtu¬miaji anafika sehemu ambayo wateja wetu wananufaika na ushauri wa kitaalamu kuhu¬su thamani ya bima inayotolewa na wafan¬yakazi wetu waliopata mafunzo mazuri.**
>
> **"Mtu anaweza kuuliza 'kwanini benki zina¬taka bima'. Afya na hali nzuri hya wateja wetu ni muhimu kwetu, kwa kuwa ni kwa ajili hya kulinda vitu na mali zao. Kwa hiyo tunachanganya nia hii na fursa inayokuja nayo pamoja na mabadiliko ya sharia am¬bayo yanawezesha benki kutoa huduma za bima,"**
>
> **KAULI YA RUTH ZAIPUNA, AFISA MTENDAJI MKUU WA NMB BANK WAKATI BENKI HIYO IKIZINDUA HUDUMA YA BANCASSURANCE MWAKA 2020.**

**Nguvu ya Kifedha**

NMB Bank pia hailengi kuwa kina¬ra katika huduma ya bancassurance pekee, bali pia ina nguvu ya kifedha ya kusukuma ajenda ya kitaifa ya ujumuishaji wa huduma za bima.

Kitu kingine kikubwa kilichob¬adili soko ambacho kimeletwa na huduma ya bima ya benki ya NMB ni malipo ya haraka ya madai, ambayo yalikuwa moja ya sababu zilizowa¬zuia watu kukata bima.

Wahanga wa tukio la kuungua kwa soko la Kariakoo Julai mwaka 2021 wanajua kuwa ndani ya wiki mbili baada ya bidhaa zao kuteke¬tea, NMB iliwezesha malipo yao ya Sh438.4 milioni, ambayo shirika la Reliance Insurance liliwafidia kuto¬kana na hasara hiyo.

Mpango wa benki hiyo wa kufanya malipo ya ndani ya muda mfupi baa¬da ya madai kuwasilishwa (TAT) pia umenufaisha waathirika wengi wa majanga ya moto ya hivi karibuni nchini na maelfu ya waliokata bima hiyo wanaofikia sifa za kulipwa.

"Kwetu NMB, tunayo muda mfupi sana wakopokea na kuhudumia madai (tight turnaround time (TAT)), hi ndio mmojawapo ya faida kubwa tulizo zileta kwenye sekta ya bima Tanzania kitu ambacho mashirika ya bima tunao shirikiana pia wameboresha zaidi," Bw. Massawe aliongeza.

**Insurance Premium Finance**

Kuhusu kitu gani kingine kinai¬fanya NMB Bancassurance kuwa na umaarufu huu, Massawe alisema ni miradi yake mizuri kama Insurance Premium Finance (IPF), ambayo inawezesha wateja kulipa bima kwa mafungu.

IPF ni bidhaa ya mkopo iliyobuni¬wa kuwezesha wateja kufanya mali¬po yanayotakiwa na taasisi za bima bila ya kuvuruga mapato yao kwa kuwawekea riba ndogo.

Massawe alisema mkopo wa muda mfupi kwa kiasi kikubwa ume¬ondoa mahitaji ya kufanya malipo makubwa na kuepuka gharama kati¬ka kumlipa mteja.

## Bima ya maisha: Nafasi ya Bancassurance

"Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021, jumla ya fedha zilizokusanywa na mawakala kwa ajili ya huduma ya muda mrefu ya bancassurance ilidikia Sh24.4 bilioni, ikiwa imechangia asilimia 66.7 ya fedha za bima katikam¬sekta hiyo.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) itaendelea kujikita katika kuboresga usimamizi katika eneo la bima ya kutumia benki kwa ajili ya kuhakikisha sharia zinafuatwa, pamoja na kuwezdesha mikakati kwa ajili ya kuendeleza biashara ya bancassurance ili ichangamke zaidi na kuwa chombo cha kati chenye ufanisi,"

## Martine: Kazi yetu ni kukidhi mahitaji yako yote ya bima

**Mwezi Mei 2019, enzi mpya ya bima ilianza nchini baada ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) kuchapisha kanuni zinazoruhusu benki kuendesha biashara ya bima, ambayo inajumuisha benki kuuza vifurushi vya bima kama mawakala wa mashirika ya huduma hiyo.**

**Februari 19, 2020, NMB Bank Plc ilianzisha huduma yake ya utoaji huduma ya bima kwa njia ya benki (ban¬cassurance) baada ya kuwa benki ya kwanza kupewa leseni na TIRA ya kufanya biashara hiyo.**

**Katika mahojiano haya, mtaalamu mwandamizi wa bancassurance wa NMB, *MARTINE MASAWE* (pichani), anaelezea tofauti ambayo chaneli mpya za utoaji bima inaonyesha katika soko na sababu za suluhisho la huduma ya bima ya benki hiyo inavyokubalika. Soma Zaidi...**



**Swali: Kwanza na muhimu, kwa kifupi tueleze mkakati wa NMB Bank katika kutoa huduma za bima na nini kilisababisha muingie katika mpango wa biashara ya bancassurance.**

**Jibu:** Kwa kuzingatia jitihada za serikali kuongeza upatikanaji wa bima nchini, NMB Bank iliona ni sahihi kuingia katika kuunga mkono ajenda ya taifa ya ujumuishaji wa bima pamoja na kusaidia kufanya mapinduzi katika huduma za bima kwa kutumia mbinu za kibunifu zinazosaidia wateja na ambazo zinapa¬tikana kirahisi.

Mkakati wetu mkubwa katika biashara hii unalenga katika kuunda dirisha moja ambalo wateja wetu wata¬pata huduma zote za kifedha. Tunataka kufanya upatikanaji wa huduma za bima nchini Tanzania kuwa miongoni mwa njia rahisi katika masuala binafsi ya kifedha kwa kutumia mtandao wetu mpana wa matawi na chaneli za kibunifu za kidigi¬tali.

Kwa sasa sisi ndio pekee tunaouza bima kwa kutumia namba ya USSD ya *150*68#. Na hii ni kwa wateja wa NMB na wasio wateja wa NMB ambao wanaweza kuitumia bila ya kujali mtandao wao wa simu wanaotumia.

**Nani ni washirika wa NMB katika huduma ya bancassurance na umuhimu wa ushirikiano huu ni nini kwa wateja na wananchi kwa ujumla?**

Kanuni za bancassurance zinaitaka benki kushirikiana na mashirika ya bima yasiyozidi kumi kuweza kufanya biashara hii. Kwa kuzingatia hilo, NMB Bank Plc imeshirikiana na kampuni kumi bora, ambazo zimeshika sehemu kubwa katika soko, ambazo ni Reliance Insurance, Jubilee, Alliance Life, Britam Tanzania, Metro Life Assurance, Sanlam, Shirika la Taifa la Bima (NIC), UAP Insurance, NHIF na Shirika la Bima la Zanzibar.

Umuhimu wa ushirika huu ni ush¬indani wa washirika wetu katika kutoa huduma bora, uwezo wao na unyumbufu katika kufanya malipo ya madai, jambo linalowezesha wateja wetu kupata bima zao katika tawi la NMB lililo karibu yao kabisa.

Kwetu NMB Bank, hatuna uchelewe¬shaji na tunaendana na muda una¬otakiwa (Turn Around Time, TAT) wa malipo ya madai, jambo ambalo ni moja ya manufaa tuliyoingiza katika sekta na viwango ambavyo ni lazima washirika wetu wavifikie, kitu ambacho wamekuwa wakikifanya.

**Unakubaliana na hoja kwamba ili¬kuwa ni ukosefu wa njia bora za kibu¬nifu za uuzaji wa bima kama hii ya NMB Bancassurance ambao ulifinyi¬sha ukataji bima, kudumaza ukuaji wa sekta na kuwa tatizo katika kuchang¬ia harakati za ujenzi wa taifa?**

Hilo linaweza kuwa moja ya sababu kwa kuwa chaneli za uuzaji bima zilipa¬tikana katika majiji na miji mikubwa tu. Lakini benki zilisambaa na mfano mzuri wa hilo ni NMB Bank, ambayo kwa sasa iko katika kila wilaya Tanzania.

Kwa hiyo, kuwa na huduma ya bima kwa njia ya benki ni hatua kubwa katika sekta kwa kuangalia kuboresha upa¬tikanaji wa huduma. Nina uhakika tut¬aona chaneli zaidi za ubunifu za aina hii kadiri serikali itakavyoendelea kuboresha mazingira ya uendeshaji.

NMB Bancassurance, ikiwa na matawi 226, imewezesha bima kujipenyeza na kufikia maeneo ambayo kampuni za bima hazikuweza kufika. Mbali na njia hizo, NMB ina chaneli nyingine za usam-bazaji. Hizo zinajumuisha huduma kama NMB Mkononi, mawakala (NMB Wakala), huduma ya benki kwa njia ya internet (internet banking) na NMB Mkononi Plus.

Zote hizi zitatumika kusambaza huduma ya bima mara tu sheria zitaka¬poruhusu Tayari, NMB Mkononi Plus inafanya hilo na muda mfupi ujao tovuti itafunguliwa kufanya kazi hiyo wakati tukisubiri idhini kwa mawakala wetu ili pia waanze kuuza vifurushi vya bima.

**Kwanini na kwa jinsi gani NMB Bank ni bora zaidi ya wengine na imejipangaje kimkakati kuwa kinara katika soko la bima kwa njia ya benki na nyota inayong'aa katika kuongoza juhudi za serikali kuongeza upa¬tikanaji wa bima nchini?**

Kwanza, ni uwezo wa kibunifu wa benki katika uendelezaji bidhaa, ambao unashughulikia mahitaji ya wateja na maendeleo ya kiteknolojia ambayo yanai¬weka NMB juu katika ushindani sokoni.

Kitu kingine kikubwa ni mfumo wetu wa kipekee wa bancassurance, ambao pamoja na mambo mengine, unahakiki¬sha upatikanaji wa huduma kwa wakati na usimamizi sahihi wa taarifa za wateja. Pia tuna mtandao mpana wa matawi kuliko benki zote. Mtandao huu humpa mteja uhakika wa upatikanaji huduma zetu za bima katika tawi lililo karibu yake.

Muhimu zaidi ni jina lenyewe la NMB. NMB ni benki inayoaminika yenye wigo mpana wa wateja. Kwa hiyo benki haina budi kuendeleza heshima yake kwa kutoa huduma bora kwa wateja.

Huduma za bancassurance za NMB zinauzika kama njugu. Kwa kifupi elezea ubora ulio nyuma ya umaarufu wa vifu¬rushi kadhaa.

Kitu muhimu katika suala hilo ni kuwa na bidhaa za bima ambazo zimebuniwa kwa kuzingatia hali halisi ya kiuchumi katika soko la Tanzania.

Masuala haya yanazingatia changa¬moto za kifedha zinazowakabili wananchi wengi na yanajumuisha si bidhaa ya Bima ya Vikundi (Group Funeral Cover) pekee, pia huduma zilizoanzishwa hivi karibuni za bima ya moto kwa wafan¬yabiashara wadogo (Machinga Fire Insurance) na ya sekta ya uvuvi inayoju¬likana kama Jahazi.

Miongoni mwa mengine mengi, bima ya vikundi inashughulikia malipo ambayo yanatakiwa kutolewa wakati mwanakikundi anayechangia anapofariki au kupoteza ndugu katika familia kama mke, watoto pamoja na wazazi.

Bima ya Machinga imeundwa kwa kushirikiana na Reliance Insurance baada ya moto ulioibuka hivi karibuni katika masoko makubwa kuteketeza bidhaa za wafanyabiashara wadogo na pia imezingatia unafuu. Bei zimepangwa vizuri kati ya Sh 10,000/- na Sh 60,000/-.

Kuridhisha wateja ni kitu muhimu katika biashara hii. Bancassurance inatoa uhakika wa kuuza bidhaa za bima ambazo zimebuniwa kulingana na mahitaji ya wateja. Kitu kingine muhimu ni unafuu. NMB Bancassurance inaweka uhakika wa bei nafuu zenye manufaa makubwa kulingana na ununuzi.

Pia tunahakikisha upatikanaji rahisi kwa kuhakikisha bidhaa zote na huduma za washirika wetu zinaweza kupatikana katika tawi letu lolote. Soko na sifa za kibiashara za washirika wetu pia zime-kuwa ni faida ya ziada.

Pia muhimu ni malipo kwa wakati dhidi ya madai ya wateja. Mashirika ya bima tunayofanya nayo kazi yanal¬ipa madai yote yanayostahili kwa kasi ambayo haijawahi kutokea katika historia ya bima Tanzania. Naamini kuwa tuna TAT bora katika soko.

168927

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uwekezaji bil.78/- za sukari, mafuta una neema ya ziada

**JUZI** alipotimiza mawasilisho yake ya mapato na matumzi ya Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aligusa mambo kadhaa yanayogusa hali ya uchumi na matumizi ya serikali na taifa kwa jumla.

Alifahamisha sura kamili ya matumizi ya serikali ina mambo 10 yanayoishikilia ambayo katika namna yoyote hayakwepeki, yakitafuna wastani wa asilimia 82 ya matumizi hayo.

Kimsingi, imegawanyika kwa sura kuu tatu, ikikamata ulipaji deni la taifa na mishahara ya serikali; ujenzi wa miundombinu ya reli na barabara; pia huduma muhimu kwa umma, maji, afya na elimu.

Sasa, kurejea hiyo wastani wa asilimia 17 inayobaki ni mahsusi kutumikia mahitaji mbalimbali ya umma, ambayo ni mtambuka kisekta na aina zake. Hiyo inabeba maana gani?

Ndani ya wajihi wa bajeti hiyo inayoishia mwezi huu, inaakisi ujumbe kwamba hata baadhi ya mambo yaliyoahidiwa kufanyika katika mwaka ujao wa fedha unaotarajiwa kuanza wiki kadhaa kutoka sasa, yanaangukia katika mkondo huo.

Juzi Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Nchemba, aliliambia Bunge kwamba serikali imeamua kufanya uwekezaji mkubwa katika uzalishaji sukari kitaifa, sambamba na mafuta ya kupikia nchini.

Ni hatua inayobeba kile ambacho kimekuwa kikichukua sura ya madai ya umma katika hilo, kwamba mafuta ya kula na sukari yanayozalishwa nchini hayatoshelezi mahitaji ya umma, ilhali mahitaji yake yanapatikana ndani ya nchi.

Maana iliyoko katikati ya mstari, ni kwamba kuna haja ya kuwepo uwekezaji mkubwa nchini, ili kujiongezea uwezo wa kuziba pengo hilo lililopo la mlo muhimu na wakati huohuo inakidhi mahitaji ya jamii; chakula na unyeti wake kiafya.

Serikali imetangaza inawekeza fedha Sh. Bilioni 78 kupitia benki mbalimbali za biashara nchini kuanzia mwaka ujao wa fedha, ili kufungua milango kwa wawekezaji kupanua uzalishaji katika eneo hilo.

Ni hatua inayoashiria mwitikio wa serikali katika malalamiko ya wananchi, ambayo hapo awali Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na baadhi ya mawaziri, wamekuwa wakiahidi hatua kadhaa zitachukuliwa.

Hiyo imeenda sambamba na kushuhudiwa baadhi ya vyombo vya umma vikichukua hatua za awali, mathalan Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), hasa katika kambi yake ya Bulombora mkoani Kigoma kunakolimwa michikichi kwa wingi, ili pashuhudiwe uzalishaji mawese kwa wingi, hata kuchangia kuziba pengo la uhaba wa mafuta ya kula.

Aidha, askari wenzao jeshi la Magereza, nao wanazama katika uzalishaji alizeti, mazao yote kwa jumla yakitoa mafuta ya kula. Tabasamu nyingine ya umma inayotarajiwa ni kwamba, matunda ya miradi hiyo inayowekezwa kutoka Sh. bilioni 78 hizo za serikali, itakuwa sehemu ya mwitikio wa kilio cha ajira kwa vijana wanaoteseka.

Lingine linaloendana nalo, ni kwamba mzunguko wa pesa ndani ya nchi kuwa juu, hali inayohitajika sana kiuchumi kukuza biashara, ikiziibua sekta nyinginezo na shughuli za kiuchumi. Ni kawaida huwa zinategemeana na kuiinua katika kile wanachokiita wachumi 'multiplier effect.'


Hapo maana yake ni pana. Kutakuwapo uzalishaji mkubwa wa sukari na mafuta ya kula, pia kutadhibiti mfumuko wa bei ama kwa kuupunguza kutoka tulipo au kuuondoa kabisa.

Uagizaji bidhaa za nje ya nchi utapunguzwa na Watanzania watabaki wakitabasamu kuona ajenda yao ya Uchumi wa Viwanda inachukua nafasi, wakiviona viwanda vingi vya mafuta ya kula na sukari.

Sisi Nipashe tunaikaribisha kwa mikono miwili ajenda hiyo ya kuwekezwa Sh.bilioni 78, kwani tukivalia miwani tunaona mengi ya neema yanakuja nayo, hata kufikia nafasi yetu tulipo na wenzetu wengi wa sekta tofauti.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Beauty Fred Mwakatobe, TUDARCo

# Tuwape ujasiri watoto wetu kukabili madhila ngono yanayowakuta mitaani

**MTU** unapoperuzi kwenye mitandao ya kijamii au vituo vya habari nchini, kwa sasa si ajabu katika taarifa tano mbili au tatu, zikawa za ukatili wa kingono kwa watoto wadogo (wa kike na kiume).

Ni tofauti kabisa na zamani, miaka ya nyuma matukio haya hayakuwapo sana kutokana na wazazi walikuwa walizi namba moja kwa watoto wao. Hivi sasa matukio haya yamekuwa mengi kutokana na sababu mbalimbali.

Moja, wazazi wengi wapo 'bize' sana kwenye kutafuta pesa na kusahau jukumu la kuwalea watoto kuwa ni lao, pia badala yake wanawaachia jukumu hilo wafanyakazi wa majumbani. Hiyo imekuwa tatizo kubwa sana la watoto kufanyiwa ukatili wa kingono, kama vile kinajisiwa huku wakubwa wao nao wanabakwa na kulawitiwa na watu wa karibu sana kifamilia, bila ya wazazi wao kugundua mapema.

Watoto wanakosa elimu ya kulinda afya zao dhidi ya watu wabaya, kutokana na kukua kwa utandawazi kwa sasa ni vyema watoto wangepewa elimu dhidi ya viashiria viovu vya kumwingiza kwenye matendo ya kingono na pindi ikitokea hali hiyo au kiashiria chochote cha vitisho juu ya kushiriki ngono na mtu yoyote hata kama ni ndugu au mtu yoyote anayefahamika nyumbani.

Hiyo imeenda mbali zaidi na kuhusishwa na imani potofu za kishirikina, waganga wa kienyeji wanawapa masharti ya kutekeleza haja ya kingono kwa watoto wenye umri mdogo sana, ili waweze kufanikiwa kwa kile walichodhamiria kukipata, ikiwamo kupata utajiri wa haraka.

Wengine wananufaika kushiriki vitendo hivyo vya kikatili kwa watoto wao wa damu hata watoto wa ndugu zao wa damu, wengine hutekeleza matukio haya hata watoto wa majirani zao.

**Wengine wananufaika kushiriki vitendo hivyo vya kikatili kwa watoto wao wa damu hata watoto wa ndugu zao wa damu, wengine huteke leza matukio haya hata watoto wa majirani zao.**

Usugu huo wa matukio ya kikatili kingono kwa watoto, kimsingi yamezidi kushamiri kwa kasi, kiasi kwamba hata walimu wenye dhamana ya kuwapa elimu watoto hao huwafanyi shambulio la aibu, kwa kuwashawishi kushiriki nao matendo hayo ya kikatili kwa watoto wadogo sana kama inavyoripotiwa na mamlaka mbalimbali zinazohusika.

Ningependa kuipongeza serikali iliyoko madarakani chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada za kuibua maovu hayo na adhabu wanazopewa watuhumiwa wanaofanya ukatili huu wa kingono kwa watoto wadogo.

Pia natoa rai kwa mamlaka husika zinazopambana na ukatili wa kingono hasa wa watoto kutilia mkazo zaidi kwenye kutoa semina za mafunzo kwa wazazi na walezi juu ya kuwalinda watoto dhidi ya matukio hayo ya kikatili, ili wasiharibu dira ya mafanikio ya watoto wao.

Elimu inapaswa itolewe shuleni na iwafikie walengwa ambao ni watoto, hasa kwa kuwapa ujasiri wa kuripoti matukio hayo yanapowakuta, pasi kujali vitisho kwa wanaotekeleza matukio hayo. Vivyo hivyo, waepuke vishawishi vya kupewa vitu, ili wakashiriki tendo la ngono katika umri huo mdogo walio nao.

Na mpango huu wa kupunguza na kutokomeza matukio ya kikatili ya kingono kwa watoto, utafanikiwa endapo jamii wazazi na serikali wakishirikiana kwa pamoja, hasa wazazi wa kike wanatakiwa kupata muda mwingi wa kuzungumza na watoto wao wa kike kwa wa kiume na kuwaweka wazi juu ya hali ya dunia kwa sasa ilivyo, hawataki kuwaamini watu ovyo, hata kama ni ndugu.

Kimsingi, wanapaswa wachukue hatua hata pale, anatokea mtu yoyote anayeonyesha dhamira ya kumfanyia ukatili wa kingono, awe huru kuripoti kwa mtu sahihi bila ya kuogopa vitisho alivyopewa na mtu aliyetekeleza au anayetaka kutekeleza mambo hayo machafu.

## Benki yatoa madawati kwa shule ya msingi

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Mtongani iliyopo Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam, sasa watasoma kwenye mazingira bora baada ya Benki ya I&M kutoa msaada wa madawati 100 ambayo yatanufaisha wanafunzi 300 pamoja na vifaa vya usikivu 50 kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia.

Vilevile, wanafanyakazi wa benki hiyo wameungana kutoa msaada kwa vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi wenye uhitaji wa shule hiyo.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 12.5 ulipokewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, kwa niaba ya Shule ya Msingi ya Mtongani.

Msaada huo kutoka kwa Benki ya I&M ni muendelezo wa kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha wanafunzi wanapata masomo yao kwenye mazingira rafiki.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Mkuu wa Kitengo cha Biashara Benki I&M, Lilian Mtali, alisema msaada huo una lengo la kutengeneza fursa kati ya wafanyabiashara na jamii inayozunguka.

"Fursa siyo kwa ajili ya fedha tu, ni kutengeneza maisha ya baadaye kwa watu pamoja na jamii sehemu yoyote duniani," alisema Mtali.

Aliongeza: "Maono ya Benki ya I&M ni kutoa hamasa na kusaidia kubadilisha maisha ya Watanzania kila siku. Tunafanya biashara kwa njia sahihi na kwa ajili ya maisha ya baadaye, msaada huu kwa Shule ya Msingi Mtongani utawapa nafasi ya mafanikio kwenye elimu yao."

Alisema ushirikiano baina ya sekta binafsi, serikali pamoja na taasisi zisizo za serikali ni njia bora ya kutatua kero zinazokabili maisha ya Watanzania.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate, alisema msaada huo unaonyesha ushirikiano mzuri uliopo baina ya Serikali na sekta binafsi, ambao kwa kiasi kikubwa umenufaisha jamii kwa kuwa madawati hayo yatatatua kero kwa wanafunzi kukaa chini ambayo ilikuwa inawakabili kwa muda mrefu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mtongani, Victor Kangahti, alishukuru Benki ya I&M, akisema msaada huo umekuja muda mwafaka kwa kuwa shule hiyo ilikuwa inakabiliwa na uhaba ya mawadati kufuatia ongezeko la wanafunzi baada ya Serikali kuanza utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo, maarufu elimu ya bure.

"Kwa niaba ya uongozi wa shule yetu, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Benki ya I&M kwa msaada huu kwa shule yetu. Mimi kama Mkuu wa Shule hii, naomba niwahakikishie ya kwamba msaada huu wa madawati utatumika vyema kama ilivyokusudiwa pamoja na kutunza vizuri kwa ajili ya wanafunzi waliopo kwa sasa na kwa wale ambao watakuja kwa baadaye," aliahidi.

# Mwalimu mazoezi mbaroni tuhuma kunajisi mwanafunzi

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

ALIYEKUWA mwalimu wa mazoezi katika Shule ya Msingi Mkombozi, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Abel Bulugwe (21), anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe kwa tuhuma za kumnajisi mwanafunzi wa darasa la sita (11) anayesoma katika shule hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio hilo lilitokea Juni Mosi majira ya saa 12 jioni.

Kamanda alisema mwalimu huyo alikwenda shuleni huko kwa ajili ya kufundisha ikiwa ni mafunzo kwa vitendo baada ya masomo yake katika Chuo cha Ualimu Tandala kilichoko wilayani Makete mkoani Njombe.

Alisema mwalimu huyo alifundisha kwa kipindi cha miezi miwili kuanzia Januari mwaka huu kisha kurejea chuoni kuendelea na masomo yake mpaka alipomaliza.

Alisema mwanzo mwa mwezi Juni mwaka huu, alionekana mjini Njombe na ndipo alipokutana na mwanafunzi huyo amembeba mtoto akiwa anaelekea saluni kunyoa. "Alimsindikiza mwanafunzi huyo mpaka saluni na matokeo yake mazungumzo yakawa mengi na kufikia hatua mwalimu huyo kuondoka na mwanafunzi huyo mpaka sehemu alipofikia ambayo ni kwa rafiki yake," Kamanda Issah alisema.

Alisema mwanafunzi huyo alilala huko kwa mwalimu huyo pamoja na mtoto aliyekuwa naye na hivyo kushindwa kurudi nyumbani siku hiyo na kupelekea watu wanaoishi katika mtaa wake kuanza kumtafuta na baadaye Mwenyekiti wa Mtaa alimwona na kutoa taarifa.

Alisema kufuatia taarifa hizo , mwalimu huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi wakisubiri taratibu zingine za kisheria zifuatwe ili afikishwe mahakamani kutokana na kosa linalomkabili.

Alitoa wito kwa wazazi kuwa makini na watoto wa kike ambao wamepevuka, wasiwe wanaondoka nyumbani bila ya kujua walipo na ikiwezekana watoe taarifa ili kukabiliana na matukio hayo ya kikatili.




Mkuu wa Kitengo cha Wajasiriamali wa Benki ya NBC, Mussa Mwinyidaho, akizungumza na wageni waalikwa wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo, kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa wa mkoani Manyara hivi karibuni, ili kujadili fursa za biashara, kutambulisha huduma mpya za benki hiyo kupitia huduma yake ya NBC Biashara Club. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wafanyabiashara itumieni Benki ya Exim kuwekeza'

**Na Mwandishi Wetu,**
TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burian, amewaomba wafanyabiashara mkoani humo kuhakikisha wanachangamkia uwapo wa taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Exim mkoani humo kwa kufanya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi ili kuuendeleza mkoa huo.

Akizungumza wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa wa mkoani hapa juzi, Balozi Dk. Burian alisema bado wakazi wa mkoa huo hawajatumia kikamilifu uwapo wa taasisi hizo katika kujikwamua kiuchumi wao binafsi na faida ya mkoa kwa ujumla.

"Mkoa wa Tabora upo kwenye uchumi unaokua. Ili kufanikisha ukuaji wake, tunahitaji sana wawekezaji kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kilimo, ufugaji na viwanda ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi wetu.

"Ni sisi kama wana Tabora ndiyo tuna jukumu hilo tusisubiri watu watoke mikoa mingine kuja kufanya jambo hilo hapa. Na Benki ya Exim wapo hapa leo kutukumbusha hilo, hivyo nachoomba ni ushirikiano wenu mchangamkie huduma zao ikiwamo mikopo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua mkoani humo, Paul Chacha, alisema kupitia huduma ya Exim Wakala, wakazi wa mkoa huo wanatarajia kuchangamkia zaidi huduma za kifedha kupitia benki hiyo kwa kuwa awali walishindwa kufanya hivyo kutokana na wananchi katika maeneo mengi kushindwa kufikiwa na huduma za benki hiyo.

"Mwaka huu tunatarajia kuvuna tumbaku kiasi cha zaidi ya kilo milioni 10, hivyo tunatarajia huduma nzuri pia za kifedha. Ujio wa Exim Wakala utakuwa ni mkombozi kwa wananchi wa Tabora ambao licha ya kuvutiwa na huduma za Exim muda mwingine wamekuwa wakishindwa kuitumia vyema benki hii kwa kuwa walikuwa hawafikiwi na huduma zake kwa ukaribu zaidi," alisema.

Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo, alisema benki kwa sasa inauweka Mkoa wa Tabora katika vipaumbele vyake kwa kuhakikisha zaidi huduma zake katika mkoa huo zinakwenda sambamba na mkakati wa mapinduzi ya kiuchumi ya mkoa huo.

"Tumebaini kwamba kwa sasa Mkoa wa Tabora unapitia mabadiliko makubwa ya kiuchumi katika maeneo mbalimbali ikiwamo biashara na kilimo ambayo yanahitaji ushiriki mkubwa wa taasisi za kifedha na hivyo Benki ya Exim tupo tayari kwa ushirikiano mkubwa katika kufanikisha hilo.

"Ujio wa huduma yetu ya Exim Wakala unalenga kufanisha hilo zaidi, hivyo tunaomba sana wana Tabora mtupokee," alisema Lyimo.

Baadhi wa wafanyabiashara mkoa huo walisema wakati mkoa huo ukiwa unajipanga kujenga uchumi imara na endelevu, ufanisi katika mfumo wa fedha ni moja ya mahitaji ya muhimu kwao ili waweze kushiriki katika ukuaji wa uchumi huo na maendeleo kwa ujumla.

"Ndiyo maana leo tumeshukuru sana kuona Benki ya Exim imetuita hapa kututangazia kwamba ipo pamoja na sisi katika kufanikisha hili. Tunawashukuru sana kwa hilo na sisi tupo tayari watupokee," alisema Snega Juma, mmoja wa wafanyabiashara mkoani humo.

# 'Itungwe sheria kali zaidi mikopo ya halmashauri'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Erasto Makala, ameiomba serikali kuandaa sheria kali kwenye utoaji wa mikopo ya asilimia kumi, ili kuwadhibiti wanaokwamisha urejeshaji kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mjini Mlandizi baada ya kikao cha Baraza la Madiwani, Makala alisema baadhi ya vikundi vilivyonufaika na mikopo hiyo havijarejesha, hivyo kukwamisha wahitaji wengine kunufaika.

Alisema endapo zitawekwa sheria kali zitasaidia kuondoa vikwazo vilivyoko sasa ambavyo vinasababisha vikundi vinavyohitaji kushindwa kupatiwa mikopo hiyo kunakosababishwa na watu wachache ambao hawajarejesha.

Makala alisema kutokana na hali hiyo halmashauri imejipanga kuchukua hatua za makusudi kwa wadaiwa ambao wanakwamisha malengo yaliyowekwa ya kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mikopo kwa wakati.

"Mikopo hii siyo hisani, anayekopa anatakiwa kurejesha ili wengine wanufaike na madiwani wasiwatetee hawa wanaodaiwa bali wasimamie taratibu ili malengo ya halmashauri ya kuyawezesha makundi yanayolengwa yafikiwe," alisisitiza.

Mwenyekiti huyo alisema wameshatoa maagizo kwa watendaji wa kata kuhakikisha wanachukua hatua kwa vikundi vilivyokopa virejeshe fedha hizo, lakini wametoa miongozo kwa maofisa maendeleo ya jamii kushughulikia suala hilo kwani linasababisha kuwapo kwa hoja kwa wakaguzi wa hesabu za ndani na nje.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ruth Mwelo, alisema vikundi vinavyopata mikopo vinatakiwa kupata elimu kuhakikisha wanarejesha fedha za mikopo kwa kuweka benki na siyo kuwapatia watumishi wa warejeshee.

Alisema watumishi wanaosimamia urejeshaji wa mikopo hususani wa maendeleo ya jamii ngazi ya kata wanatakiwa wahakikishe wanakuwa waadilifu, waaminifu kwa mujibu wa sheria kwa kufanya kazi kwa kufuta taratibu kwa kutopokea fedha za vikundi za marejesho kutoka kwenye vikundi.

"Hairuhusiwi mtu yoyote hata kama ni msimamizi wa mikopo kupewa fedha mkononi kwasababu baadhi yao wamekosa uaminifu wa kurejesha fedha hizo benki na hivyo kufanya halmashauri kupata hasara.

"Na hii ya kuwapatia wataalamu imesababisha baadhi ya vikundi kuonekana bado vinadaiwa wakati fedha wamewakabidhi wataalamu jambo ambalo ni kinyume na taratibu," alisema.

Ruth alisema wakati mwingine hali hiyo inasababisha halmashauri kupata hasara pale fedha hizo zikiwa hazirejeshwi na wengine kukosa fursa ya kukopa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma ya Jamii, Josephine Gunda, alisema wadaiwa wa mikopo ya halmashauri wanatakiwa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ili vikundi vingine vinavyohitaji kukopa vinufaike kwa wakati.

Gunda alisema ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo inatakiwa kuwachukulia hatua ili kukomesha tabia hiyo ambayo inawanyima wengine kunufaika.




Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Latifa Mohamed Hamis, wakitiliana saini makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi hizo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ofisa kilimo kizimbani tuhuma za ubadhirifu

**Na Samson Chacha**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mara imemfikisha mahakamani Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Sixtus Alfred kwa tuhuma za ubadhirifu na ufujaji wa mali ya umma zenye thamani ya Sh. milioni 8.01.

Akisomewa mashtaka hayo mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Serengeti, Jacob Ndira, Mwanasheria wa TAKUKURU, William Lyamboko, alidai kuwa mtumishi huyo akiwa mtumishi wa Idara ya Kilimo ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti mkoani Mara alifanya ubadhirifu na ufujaji mali ya umma zenye thamani ya Sh. milioni 8.01. Alisema ubadhirifu huo aliufanya kati ya mwaka 2019 na 2021 kwa kutumia mashine za kukusanya fedha kinyume na kifungu cha 28, (1) PCCA pamoja na kifungu cha 57 (1) na 60 (2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi.

Hata hivyo, mtuhumiwa huyo baada kusomewa mashtaka hayo alikana kuhusika na kuomba dhamana, kwamba alitimiza masharti aliyopewa, kesi hiyo itatajwa tena Julai 5, mwaka huu.

Katika kesi nyingine katika mahakama hiyo, TAKUKURU ilimfikisha mahakamani hapo mtumishi wa Idara ya Maji MUGUWASA, Godwin Nyigana, kwa makosa mawili ya kuomba na kupokea rushwa.

Mwanasheria wa TAKUKURU, William Lyamboko, alidai kuwa mtuhumiwa huyo akiwa mtumishi wa Mamlaka ya Maji MUGUWASA, Mei mwaka huu aliomba na kupokea Sh. 40,000 kutoka kwa mteja aliyehitaji huduma ya maji, kwamba aliwekewa mtego na kukamatwa akiwa na fedha hizo.

## Kafulila ampa siku saba mkandarasi

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ametoa wiki moja kwa mkandarasi AUDACIA INVESTIMENT LTD anayetekeleza mradi wa upanuzi wa maji Nkololo, kuhakikisha analeta mabomba ya kukamilisha mradi huo.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha siku 16 kuanzia sasa.

Alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa mkoani humo ikiwamo ya RUWASA na TARURA.

Kafulila alisema kuwa ujenzi wa mradi huo wa upanuzi wa mradi wa maji hauridhishi na kwamba mpaka sasa umefikia asilimia 15 kati ya asilimia 100 alizopaswa kukamilisha kwa muda wa miezi sita.

"Natoa wiki moja mkandarasi ahakikishe anafikisha na kusambaza mabomba hayo kwenye mradi huo na endapo asipofanya hizo mkataba wake uvunjwe," alisema Kafulila.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa upanuzi wa mradi wa maji Nkololo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Bariadi, Mapengo Gendai, alisema mradi huo unatekelezwa kupitia programu ya PforR kwa muda wa miezi sita, lakini mpaka sasa mkandarasi kafikisha asilimia 15, huku muda uliosalia wa ukamilishaji ukiwa umebaki wiki mbili.

Gendai aliongeza kuwa mradi wa maji wa Nkololo unatarajia kuhudumia wakazi wapatao 6,300 ambao watapata majisafi na salama na vijiji vinavyozunguka kata hiyo vitanufaika.

Baadhi ya wakazi wa Nkololo wakizungumza na Nipashe walisema wamekuwa wakihangaika kupata maji na wakati mwingine wanatembea umbali mrefu.

Walisema kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wengi wa Nkolo ambao wamekuwa wakipata tabu kwa muda mrefu.

Ruth Sanga alisema kukamilika kwa mradi huo kutapunguza adha ya wananchi kusaka maji umbali mrefu na kuiomba serikali kumsimamia mkandarasi huyo ili amalize kwa wakati.

Mkandarasi wa mradi huo, Janeth Scrato, alisema ni matumaini yake muda aliopewa wa kukamilisha mradi huo atautumia vema kukamilisha kazi hiyo.

**"Natoa wiki moja mkandarasi ahakikishe anafikisha na kusambaza mabomba hayo kwenye mradi huo na endapo asipofanya hizo mkataba wake uvunjwe," alisema Kafulila.**

TANGAZO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## Ina Ithibati ya ISO 9001:2015

## TAARIFA KWA UMMA

### MABORESHO YA MTANDAO WA TRA

**Dar es Salaam, 08 Juni, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwataarifu wadau wake na Umma kwa ujumla kwamba, tutafanya maboresho ya mtandao siku ya **Jumapili** tarehe **12.06.2022** kuanzia **saa 6:00 usiku** hadi **saa 12:00 asubuhi.**

Maboresho hayo yataathiri upatikanaji wa mifumo yote ya TRA kama vile Tovuti ya **TRA, TANCIS, e-filing, EFDMS, TIN, Mfumo wa Malipo (RGS)** kwa watumiaji wote, Hivyo Huduma zote za mtandao hazitapatikana katika kipindi chote cha maboresho.

Baada ya maboresho hayo, maunganisho binafsi ya kimtandao baina ya TRA na wadau wake yanaweza kuathirika pia. Hivyo hali hii ikijitokeza, tafadhali wasiliana na dawati letu la huduma kwa namba **+255 786 899 900** kwa msaada na utatuzi wa tatizo lililojitokeza.

TRA inaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza kupitia maboresho hayo kwani tunatarajia yataboresha huduma tunazozitoa.
Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia WhatsApp namba **+255 744 233333** au tupigie simu namba **0800 75 00 75** au **0800 78 00 78** au **0800 11 00 16**, Barua pepe: **huduma@tra.go.tz**. au **service@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

## HABARI KITAIFA

# RC aagiza mmiliki salfa feki korosho ajisalimishe

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ametoa saa 48 kwa mmiliki wa kiuatilifu cha salfa ya unga chapa Makonde kujisalimisha kwa mamlaka ya serikali mkoani humo kwa madai ya kusambaza kwa wakulima kiuatilifu feki.

Pia amesema tayari watu saba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa kukutwa na kiuatilifu hicho mifuko 2,100 katika wilaya za Tandahimba na Newala mkoani humo.

Alibainisha jana mjini hapa kuwa watu wanne ambao ni wafanyabiashara wamekamatwa katika Wilaya ya Newala wakiwa na mifuko 1,600 na wengine watatu katika wilaya ya Tandahimba wakiwa na mifuko 500 ya kiuatilifu hicho.

"Ninatoa saa 48 kwa mmiliki wa salfa chapa Makonde kujisalimisha katika mamlaka za serikali mkoani Mtwara ili atoe ushirikiano juu ya salfa hii...baada ya huo muda atatafutwa popote alipo na kukamatwa ili atoe ushirikiano," alisema Gaguti na kuongeza:

"Hawa tuliowakamata wapo katika taratibu za mwisho kuwafikisha mahakamani... na nitoe wito kwa wakulima kutotumia pembejeo nje ya zile zilizotolewa na serikali na watoe taarifa pindi wanapoona viuatilifu wasivyovifahamu," aliagiza.

Wakati huo Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Mtwara umetoa wiki moja kwa mamlaka husika kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika na usambazaji wa pembejeo hizo feki za korosho.

Mwenyekiti wa umoja huo Mkoa wa Mtwara, Naseeb Kanduru, alisema kuwa iwapo mamlaka husika zitashindwa kufanya hivyo, umoja huo utayaweka wazi majina ya wahusika wote wa kashifa hiyo ya pembejeo feki bila kujali wadhifa wala cheo.

"Mkuu wa Mkoa tunatambua kazi kubwa unayoifanya na uliahidi siku ile kuwa utafanya wewe mwenyewe, sasa kwa kuwa ilikuwa ahadi yako na hizo 'klipu' zipo, hawa wahusika tunakuomba ushughulike nao, taarifa ya mamlaka imethibitisha zipo hizo pembejeo tunataka tuone hatua zinazochukuliwa," alisema Kanduru.

Aliongeza kuwa wao kama umoja wa vijana watakaa kimya kwa muda mfupi baada ya hapo watawataja wote waliohusika bila kuhofia vyeo vyao.

Alifafanua kuwa umoja huo utahamasisha vijana wa mikoa mingine inayolima korosho kuhakikisha pembejeo zisizofaa kwa matumizi pindi zinakamatwa na kuteketezwa ili kunusuru anguko la uzalishaji wa zao hilo nchini.

"Tunapokuwa na viuatilifu ambavyo havina ubora, fatsiri yake ya kwanza nini, uzalishaji hautafikia malengo, tusipofikia malengo uzalishaji kile ambacho tulichowaahidi wananchi hakitafikia, lakini lazima tukubaliane, Rais alisema atatoa pembejeo bure kwa wakulima," alisema Kanduru.

Mwenyekiti huyo pia aliwashukia wabunge wa Mkoa wa Mtwara kwa ukimya wao katika sakata hilo la pembejeo feki huku wakulima wakiteseka.

"Kila mbunge anaongelea suala la maji, lakini kwenye hili wapo kimya, je, hawajui? Athari zinazoenda kuwakuta wananchi wao ambao wanaowaongoza, sasa mimi niseme tunazo taarifa za kutosha za mlolongo wa watu wote wanaohusika na tunajua wapo wakubwa wengine kwenye wilaya, mkoa hadi taifa ambao hawa watu wanawashikia," alifafanua Kanduru.

# DC ampa siku saba mwenyekiti wa kijiji

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, ametoa siku saba kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Bulamata na kamati ya ujenzi kuhakikisha kituo cha afya Bulamata kinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Buswelu alitoa maagizo hayo wakati alipotembelea katika kituo hicho kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi juzi na kubaini mradi huo kusuasua.

Alisema upo uzembe kuanzia kwa mwenyekiti wa kijiji, ofisa mtendaji wa kijiji na kata na mhandisi hafuatiliwi kikamilifu, hivyo akaagiza kuwekwa taa katika eneo hilo ili kazi ifanyike mchana na usiku.

"Rais ametoa fedha zifanye kazi sio zisimame, hayupo aliye mkubwa zaidi ya Rais, atoe fedha aagize kazi ifanyike anakuwapo mmoja anakwamisha halafu haji kwenye kazi, haipo hiyo," alisema Buswelu.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bulamata alisema awali walipokea shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho ambapo walitegemea kuwe na majengo matatu likiwamo jengo la maabara.

Fundi mkuu wa mradi huo, Jailos Nyandwi, alisema mradi huo umechelewa kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo ucheleweshwaji wa vifaa na malipo ambao unapelekea mafundi wengi kukimbia.

"Kuna baadhi ya matukio kama simenti hazikufika kwa wakati, tukiuliza kamati wanadai kwamba usafiri, lakini kamati ya ujenzi wilaya inatufanya tusiende kwa kasi zaidi maana kila hatua inatakiwa tuwasiliane nao waje kukagua lakini hawafiki kwa wakati," alisema Nyandwi.

Imeelezwa kuwa kituo cha afya Bulamata kilitakiwa kikamilike Mei 23 mwaka huu, lakini mpaka sasa hakijakamilika.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burian, akizungumza na wageni waalikwa wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Benki ya Exim kwa ajili ya wateja wadogo na wakubwa wa mkoani humo hivi karibuni, ili kujadili fursa za biashara na kutambulisha huduma mpya za benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yapata mwarobaini kudhibiti vishoka wa umeme

**Na Daniel Limbe,** CHATO

SHIRIKA la Umeme nchini (TANESCO) limedai kuja na mkakati madhubuti wa kudhibiti vishoka waliokuwa wakilipaka matope na kusababisha baadhi ya wateja kutoridhishwa na huduma zake.

Katika kukabiliana na vishoka hao, sasa wateja watalazimika kuomba huduma ya kuunganishiwa umeme kwa njia ya simu badala ya kuwatumia vishoka na wengine kutumia gharama kubwa kwenda ofisi za TANESCO.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Chato mkoani Geita, Emily Ntazimila, aliyasema hayo jana baada ya kumuunganishia huduma ya umeme, Getruda Mremwa, mkazi wa Kijiji cha Zanzibar, Kata ya Bwina wilayani hapa.

"Shirika letu limekuja na mpango kabambe wa kidijitali maarufu kwa Ni-Konekt ambao unamrahisishia mteja wetu kuomba huduma ya kuunganishiwa umeme kwa njia ya mtandao... njia hii inawasaidia wateja wetu kujiepusha na vishoka ambao awali walikuwa wakiwatapeli fedha zao," alisema Ntazimila.

Ofisa wa huduma kwa wateja wa shirika hilo wilayani hapa, Salma Mbwana, alisema hakuna haja kwa wateja wanaohitaji huduma ya umeme kutembea umbali mrefu kwenda ofisi za TANESCO badala yake watumie huduma ya Ni-Konekt ambayo inapatikana kwa kuandika namba *152*00# kupitia simu ya mkononi.

"Baada ya huduma ya Ni-Konekt kuzinduliwa rasmi juzi kwenye kanda yetu maombi ya wateja imekuwa kubwa ikilinganishwa na awali walipokuwa wakilazimika kufika kwenye ofisi zetu... hata hivyo njia hii ni mwarobaini kwa vishoka waliokuwa wakijipatia fedha kwa njia ya wizi kwa wateja wetu," alisema Mbwana.

Mbali na kuonyesha furaha yake, Getruda Mremwa, alipongeza huduma ya Ni-Konekt baada ya kuunganishiwa umeme nyumbani kwake ndani ya saa 24 baada ya kuomba kupitia mfumo huo juzi.

Alilitaka shirika hilo kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili watambue huduma mpya ambazo zimeanza kutolewa na TANESCO hasa kwa wananchi waliopo vijijini.

# Serikali yachukua hatua msongamano wa magari

SERIKALI imeliarifu Bunge hatua nne ilizozichukua kwa kushirikiana na Zambia katika kuondokana na tatizo la msongamano wa magari Kituo cha Tunduma.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alibainisha hatua hizo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Momba (CCM), Condester Sichwale.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itaongeza geti lingine ndani ya Jimbo la Momba kutokana na geti la Tunduma kuzidiwa katika kutoa huduma.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chande alisema katika kurahisisha biashara kati ya Tanzania na Zambia na kuondoa tatizo la msongamano wa magari katika Kituo cha Tunduma, serikali inaendelea kuchambua na kutathmini taratibu zilizoko ili kuona kama kuna uwezekano wa kuongeza Kituo cha Forodha.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuondokana na tatizo hilo ambapo Januari 2021 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iliingia makubaliano na Mamlaka ya Mapato Zambia yanayoelekeza hatua mbalimbali za kuchukua kwa kila nchi.

"Hatua hizo ni pamoja na kuunganisha mfumo wa TANCIS wa TRA na mfumo wa ASCUDA World wa Zambia ili kuiwezesha Idara ya Forodha Zambia kupata taarifa za shehena ya mzigo husika kabla kuwasili mpakani," alisema.

Pia alisema Serikali ya Zambia itafanya maboresho ya miundombinu ya barabara na eneo la kuegesha magari kupitia ufadhili wa TMEA (Trademark East Africa).

Pamoja na makubaliano hayo, alisema serikali kwa upande wa Tanzania yenyewe imeanzisha Kituo cha Pamoja cha Forodha (One Stop Border Post, OSBP) ambacho kimesaidia taasisi zote za serikali kuwa sehemu moja na kuwasiliana kwa haraka.

"Pia serikali kupitia ufadhili wa TMEA imenunua scanners tatu ambazo ni baggage scanner, body scanner na cargo scanner."

"Aidha, baggage scanner na body scanner zinafanya kazi na cargo scanner inatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Julai 2022," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali haioni kuna ulazima wa haraka kuongeza geti lingine ili kuboresha huduma na ufanisi unaotakiwa.

"Zipo nchi nyingine ambazo tunapakana nazo, kwa mfano Kenya ina mageti ya forodha zaidi ya matatu. Je, hamwoni sasa nchi ya Zambia ambayo inahudumia nchi saba za SADC, serikali ipate geti lingine katika Jimbo la Momba kuhakikisha tunaongeza mapato?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Chande, alisema serikali inafanya uchambuzi na tathmini kupitia sehemu hiyo kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na itakapoona kuna haja ya kuongeza geti hilo litaongezwa.

# Serikali yaanza kutekeleza uamuzi Baraza la Mawaziri

SERIKALI imeanza kutekeleza maamuzi yaliyotolewa na Baraza la Mawaziri tangu Oktoba 2021 kuhusu migogoro ya ardhi kati ya wananchi na hifadhi.

Utekelezaji wa uamuzi huo ulianza katika mikoa yenye migogoro ikiwamo Mkoa wa Morogoro husussan Pori Tengefu Kilombero.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itatatua mgogoro kati ya wananchi na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) katika Bonde la Mto Kilombero.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masanja alisema timu ya wataalamu ya kitaifa ya utatuzi wa migogoro ya ardhi ipo uwandani, inaendelea na tathmini kwa kushirikisha mkoa, wilaya na wananchi wa maeneo hayo.

Alisema timu hiyo inafanya tathmini ya makazi na shughuli zenye athari kwenye uhifadhi wa vyanzo vya maji na rasilimali za wanyamapori ndani ya eneo la Pori Tengefu na Bonde la Mto Kilombero. "Utatuzi wa migogoro hiyo utaanza baada ya tathmini kukamilika," alisema.

Katika swali la nyongeza la Kunambi, alisema TAWA iliwashtaki wenyeviti wawili wa vitongoji kwa kosa la kufanya shughuli za kilimo kwenye hifadhi na Septemba 27, mwaka jana mahakama iliamuru kuachiwa huru watu hao na kurudishiwa ardhi na mali zao.

"Je, ni lini serikali itarejesha mali zao? Wananchi wa Jimbo la Mlimba ni wakulima, wafugaji na wavuvi na Tawa imekuwa ikiwasumbua mara kwa mara lini waziri atakwenda kutatua kero hizi?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Masanja alisema mtuhumiwa anapokamatwa ushahidi na mali zote hupelekwa mahakamani na inapothibitika ameshinda kesi mtuhumiwa anarejeshewa mali zake na kama zipo kwa TAWA, Serikali itashughulikia kuvirejesha kwa wakati.



Baadhi ya wabunge wakiingia bungeni, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuendelea na mkutano wa saba kikao cha 40 cha Bunge la Bajeti. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Milioni 500/- kujenga Kituo cha Afya Igusule

OFISI ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata ya Igusule.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais hiyo, Dk. Festo Dugange, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bukene (CCM), Selemani Zedi.

Katika swali lake, Zedi alitaka kujua kama serikali haioni haja ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Kijiji cha Soga ili kiwe kituo cha afya na kutoa huduma wananchi na watumishi wa mradi wa bomba la mafuta.

Akijibu swali hilo, Dk.Dugange alisema Kijiji cha Soga ni moja kati ya vijiji saba vya Kata ya Igusule yenye wakazi 23,237 na ina zahanati moja iliyopo katika Kijiji cha Soga ambayo inaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

"Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata ya Igusule," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Paresso, alisema mchakato wa kupandisha hadhi vituo vya kutolewa huduma za afya umekuwa na urasimu.

Alisema mchakato wa kupandisha hadi zahanati kwenda vituo vya afya unafanywa na wizara.

"Je, serikali haioni haja ya jukumu hilo kuliacha chini ya sekretarieti za mikoa kwa kuzingatia sifa na vigezo vile vile ili kuondoa urasimu?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dugange alisema upandishaji hadhi wa vituo vya kutolea huduma za afya ni shirikishi.

**"Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata ya Igusule," alisema.**




**Habari zote: Augusta Njoji na Salome Kitomari, DODOMA**

# ama





Ukurasa 12

**MAENDELEO NA UGUMU WAKE... Halmashauri mpya Tunduma yaelemewa na wagonjwa, sasa vitani kupata hospitali**



## Nzega kutoka ndoto za maji katika tamthilia, hadi kuwa hali halisi nyumbani

Na Mwandishi wetu

**"Haya maji tulizoea kuyaona katika picha za tamthilia za wazungu katika maonyesho ya runinga za vibandani. Haya maji ya kuoga kama mvua, tena katika bomba tuliona ni mambo ya nchi zilizoendelea zaidi na watu wengine huko nje ya nchi na miji mikubwa tu, sio hapa kwetu."** *Bi. Ndala Kapalata, Mwenyekiti wa mtaa wa Musoma, mjini Nzega anatoa simulizi hiyo.*

Bi. Ndala anaongeza kuwa jambo hilo sasa limefutika nyumbani kwake na kwa wakazi wengine wa Nzega, anaongeza sio tu kuwa maji ya kutosha yapo, bali amefunga bomba ndani ya nyumba na alichokuwa anakiona katika runinga sasa kipo katika nyumba yake, maji ya kuoga kama mvua , shower.

Mabadiliko haya katika maisha ya wananchi ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika Sekta ya Maji, kwa kukamilika kwa mradi wa maji wa Tabora-Igunga-Nzega. Mradi huu chanzo chake cha maji ni Ziwa Victoria mkoani Mwanza, wilaya ya Misungwi katika Kijiji cha Nyang'homango, kitongoji cha Ihelele. Huduma hiyo ya maji inatolewa na kituo hicho kwa saa 23 kwa siku.

Takwimu za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (NZUWASA) zinaonyesha baada ya kukamilika kwa mradi unaotoa maji katika ziwa Victoria kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji ni asilimia 98, kabla ya mradi huo huduma ya maji ilikuwa chini ya asilimia 30.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya ya Nzega Bw. Amos Kanuda anasema kuwa awali walikuwa na shida sana ya huduma ya maji, ila kwa hivi sasa Wataalamu wa Sekta ya Maji wameondosha adha hiyo, kwa kufanya kazi kubwa ambayo imemaliza kiu ya maji kwa wananchi.

Anasema kuwa watumiaji wakuu wa huduma ya maji ni wananchi na viongozi katika mitaa wanao wajibu wa kuwajua vyema wananchi wanao hitaji kupatiwa huduma ya maji, wananchi ambao tayari wanapata huduma ya maji na kusisitiza umuhimu wa kutunza miundombinu ya miradi ya maji. Hatua hii kutaifanya huduma ya maji iwe endelevu kwa wakati wa sasa na vizazi vijavyo.

Chanzo cha maji cha Ihelele, kwa mwendo wa wastani kwa gari kutoka Nzega kipo umbali utakaochukua muda wa saa tatu nanusu kufika. Hivyo, maji wanayohudumiwa wananchi wa Nzega yametoka mbali na kazi kubwa imefanywa na Serikali katika kufanikisha hilo. Chanzo cha maji cha Ihelele kina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 80 kwa siku, hivi sasa maji yanayozalishwa ni lita milioni 54, sawa na asilimia 68, kwa siku ambazo ndizo mahitaji toshelevu kwa wananchi na maeneo mengine kama viwanda.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa kwa uwekezaji uliofanywa na Serikali, endapo idadi ya wanufaika itaongezeka, hapana shaka kuwa watahudumiwa kwa kupata huduma toshelevu ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Mkuu wa Wilaya ya Nzega Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Advera Bulimba ameiongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama kutoka katika wilaya yake, kwa ziara maalumu katika kituo cha kuzalisha maji cha Ihelele, Misungwi kuona yanapotoka maji ya Mradi mkubwa wa maji wa Tabora-Igunga-Nzega. Lengo mahsusi likiwa kujifunza.

ACP Bulimba pamoja na kamati hiyo, amejumuika na Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa kutoka Nzega kujionea kazi ya uzalishaji wa maji wanayohudumiwa wananchi wa Nzega kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Nzega (NZUWASA).

Akiongea katika ziara hiyo amesisitiza kwa watendaji wa wilaya anayoiongoza kujitoa katika kuwaeleza wananchi namna bora ya kutumia huduma ya maji vizuri. Anasema hatua hii itasaidia kuepuka matumizi yasiyokuwa na lazima na kuwaepusha na gharama.

Ameweka bayana katika wilaya ya Nzega wamejipanga kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji karibu na makazi.

Kuendana na mabadiliko ya teknolojia, amesema kuwa yeye binafsi anatumia Dira ya malipo kabla, na inamsaidia kuangalia kiwango cha maji anachotumia, na fedha aliyolipia maji ikiisha anaongeza na kuendelea na huduma kwa wakati. Dira hiyo matumizi yake ni pamoja na mteja kujihudumia mwenyewe.

ACP Bulimba katoa heko kwa Serikali, kwa kuwatoa wananchi katika huduma za visima na sasa wanatumia maji kutoka Ziwa Victoria. "Serikali inapambana katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na maisha bora kupitia huduma ya Maji" Mkuu wa Wilaya ya Nzega ACP Bulimba anasema.

NZUWASA imefanikisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Nzega kufika asilimia 98, na huduma inapatikana kwa saa 24. Maji hayo yanatoka katika ziwa Victoria mkoani Mwanza kwa nguvu ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ambapo zaidi ya wananchi milioni moja wananufaika na maji hayo.

Viongozi kutoka Nzega wamefanya ziara hiyo ili wawe chachu katika kuwahimiza wananchi katika maeneo yao kutumia majisafi na salama ili kuepuka magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo salama. Pia, kuwa daraja katika kutoa taarifa kuhusu mivujo inayosababisha hasara kutokana na ukweli kuwa gharama za kuzalisha maji si haba, hivyo huduma ya majisafi lengo lake kuu ni kuwafikia wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (NZUWASA) Mhandisi Athumani Kilundumya anasema ziara ya kutembelea kituo cha kuzalisha maji ni moja ya darasa na ushirikishwaji kwa wadau wa mamlaka anayoiongoza.

Anafafanua kuwa lengo ni kujenga uelewa mkubwa kuhusu huduma ya maji na kutambua uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ili kufanikisha huduma ya maji kwa wananchi, na kuwa daraja katika kuhakikisha rasilimali maji na miundombinu ya miraji ya maji inalindwa.

"Ushirikishwa wa viongozi na jamii umeleta mafanikio makubwa hapa Nzega, mwaka 2021 upotevu wa maji ulikuwa zaidi ya asilimia 68, lakini hivi sasa upo chini ya asilimia 10 " Mhandisi Kilundumya anasema na kuongeza jamii imetambua hasara ya upotevu wa maji ambayo yangewahudumia zaidi, pia jamii inashiriki kutupa taarifa za mivujo ili tuokoe fedha inayopotea kwani gharama za kuzalisha maji ni kubwa.

Mhandisi Kilundumya anaweka bayana kuwa fedha iliyotolewa na Serikali katika mpango wa mwaka 2022-2023 imewapa nguvu NZUWASA na lengo ni kufikisha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kufika asilimia 100.

Salim Abdukadir, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya NZUWASA anasema amejionea jinsi maji yanavyozalishwa kwa kupitia hatua nyingi, hadi kupata maji bombani, na ukweli ni kuwa maji hayatoki ziwani na kuwekwa katika bomba moja kwa moja.

Abdukadir anasema kazi ya kuondoa tope katika maji, kupima maji na kuyatibu kupitia wataalamu wa maabara kwa saa 24 na kuyasukuma katika matenki ni moja ya kazi za msingi za kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama, na ni kazi inayotumia rasilimali fedha kubwa, pamoja na nguvu kazi ya wataalamu wanaohakikisha kila jambo linafanyika kwa kiwango.

Mkazi wa Nzega, Bw. Edson Kibachu anayefanya biashara ya kuosha magari anakubali kuwa maji wanayopata ni safi na salama na kuongeza matumizi ya teknolojia yameboresha zaidi huduma katika maeneo ya kazi.

Kibacha anafafanua matumizi ya Dira za malipo kabla yameleta mapinduzi makubwa kwani anajihudumia mwenyewe na kupima kiasi cha maji katika biashara, na hakuna haja ya msoma Dira tena.

Anaongeza kuwa maisha ya Nzega yamebadilika baada ya kupata maji ya uhakika, hapa tunajenga nyumba na ukiwa katika hatua ya msingi tu, tayari unaomba na kuwekewa huduma ya majisafi na mamlaka yetu. Hivyo, ujenzi unaenda vizuri na haupati tabu ya kupata maji.

Naye Arbogast Peter anayefanya biashara ya kuuza maji eneo la Gulioni anasema kabla ya mradi wa ziwa Victoria huduma ya maji ilikuwa ya mwendo wa kusuasua, na ilipatikana usiku zaidi. Anasema hivi sasa maji yapo mengi na yakutosha muda wote , na wateja hawasumbuki kupata huduma hiyo muhimu ya maji yanayoanzia ziwa Victoria hadi Nzega.

Maji wanayopata wananchi wa Nzega ni safi na salama. Hatua muhimu za kutibu maji zikishakamilika katika kituo cha Ihelele, maji hayo husukumwa kwa pampu kubwa kupitia bomba la chuma lenye kipenyo cha mm 900 hadi kwenye tanki kubwa katika mlima Mabale, likiwa umbali wa takriban kilomita 6.6. Tanki hilo la kuhifadhi majisafi na salama, lina uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha lita milioni thelathini na tano (35,000,000).

Kutoka tanki la Mabale, maji hutiririka kwa mserereko kuelekea kwa wateja katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Tabora na Mwanza. Mtandao wa usafirishaji maji unajumuisha mabomba makubwa yenye jumla ya urefu wa takriban km 700 na kipenyo kuanzia inchi 48 (mm 1,200) kwenye tangi la Mabale hadi inchi 8 (mm 200) kwenye matangi madogo.

Chanzo cha maji cha Ihelele kinasimamiwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama -Shinyanga. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA). Jukumu la mamlaka hii ni kuzalisha maji kutoka ziwa Victoria, kusambaza na kuuza maji hayo kwa jumla kwa mamlaka nyingine zinazohusika na usambazaji wa maji kwa wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini.

Mamlaka zinazo patiwa huduma hiyo ni pamoja na migodi na vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs). Wateja wa KASHWASA kwa upande wa mijini ni Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Shinyanga (SHUWASA), Kahama (KUWASA), Ngudu (MWAUWASA – Kanda ya Ngudu), Kishapu (KIWASA), Maganzo( MAGAWASA), Tabora (TUWASA), Nzega (NZUWASA) na Igunga (IGUWASA).

Kwa upande wa vijijini, KASHWASA ina jumla ya wateja 87, ambao ni Vyombo vya Watoa Huduma za Maji Ngazi ya Jamii vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Kwimba, Shinyanga, Msalala, Kishapu, Maswa, Nzega, Igunga na Uyui. Pia, Mamlaka ina Wateja watatu wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini katika maeneo ya Mwadui na Mwakitolyo. Wateja hao ni Kampuni ya Williamson Diamonds Limited-WDL, ZEMD - Mwakitolyo na Zube & Jonta Investment.

*Mkuu wa Wilaya ya Nzega Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Advera Bulimba (anayeongea) akiwa pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama kutoka katika wilaya yake, wakijionea hatua ya awali ya kutoa tope katika maji katika kituo cha kuzalisha maji cha Ihelele, Misungwi mkoani Mwanza yanapotoka maji ya Mradi mkubwa wa maji wa Tabora-Igunga-Nzega.*

Ukurasa 13

# Kunavyoshuhudiwa shida ya kunguni kwa wanafunzi shule na walio vyuoni

**Na Waandishi Wetu**

KUNGUNI ni nini? Kwa wengi si wageni nao kwa namna moja au nyingine. Ufafanuzi wa wajihi wa wadudu hao kwamba ni wadogo, hawana mabawa au katika matamshi ya kawaida, hawaruki. Rangi zao ni ama wekundu au kahawia, wakiwa na umbo la mviringo na wana miguu sita.

Ni kawaida kwa kunguni kuonekana katika rangi nyekundu zaidi, baada ya kufyonza damu ya mwanadamu, tendo analolifanya mara nyingi wakati wa usiku au karibu na mapambazuko, mtu anapokuwa amelala au kupumzika.


Kunguni ana tabia ya kuogopa mazingira yenye mwanga, hivyo wakati wa mchana hujificha kwenye nyufa za majengo na samani, dari au mbao za sakafu, nguo, magodoro na vitanda.

Lakini iwapo wana njaa, huweza kunyemelea na kufyonza damu mchana hasa kwenye vyumba vyenye giza na baada ya hapo, huwa wanarudi kwenye sehemu zao za kupumzika wakimeng'enya damu.

### WANAVYOENEA

Kuenea na kusambaa kwa kunguni, kunaweza kugawanywa katika njia kuu mbili, ya kwanza ni wao wenyewe kunguni kutambaa kutoka eneo moja kwenda jingine. Ni kwa namna hiyo, kunguni husambaa polepole.

Njia ya pili, ni pale watu wanapohamisha kunguni kutoka sehemu moja kwenda nyingine kupitia nguo za watu, magodoro, mizigo na samani.





Kunguni katika sura na mazingira tofauti. **PICHA; MTANDAO.**

Tatizo la kunguni shuleni linaelezwa vyuoni limekuwa sugu, kutokana na hali ya kuhamishika kupitia nguo za wakazi wao wanafunzi, shuka au mabegi yao, hata wakatoka sehemu ambazo zina kunguni na kuhamia ambako hapakuwapo kunguni.

### ATHARI ZAKE?

Hadi sasa kitaalamu kunaelezwa hakuna ushahidi wa uhakika wa kunguni kueneza ugonjwa huo. Ila kimsingi, kunguni wanapong'ata, husababisha mzio na hivyo kuifanya ngozi iwashe na kutengeneza vipele.

Michubuko inayotokana na kung'atwa na kunguni, inaweza kufungua mazingira ya maambukizi ya bakteria na kuunda jipu dogo, katika maeneo hayo yaliyoshambuliwa na kunguni.

Pia, upungufu wa damu kwa mtu anayeng'atwa kutokea pindi mwanafunzi atashambuliwa kila mara penye kunguni wengi.

Kero ya kuumwa na kunguni mara nyingi, hufanya wanafunzi kukosa usingizi na kushindwa kupumzika vizuri usiku.

Hiyo huwafanya kushindwa kujifunza vizuri masomo yao wakati wa mchana, kwa sababu ya uchovu, mwishoni wao huathiri ufaulu na maendeleo ya elimu ya wanafunzi wao.

### NINI KIFANYIKE?

Kuna njia za udhibiti zinazotajwa zinaweza kutumiwa kupunguza wingi wa kunguni au kuwatokomeza kabisa, pale hali ya uwepo wa kunguni shuleni na vyuoni itakapobainika.

Hapo zinahusisha kukagua kila mara dalili za uwepo wa kunguni na inapobainika wapo, hatia inayochukuliwa ni kufukiza kwa kutumia viuatilifu maalum vya kutokomeza.

Hapo inashauriwa, shule na vyuo zinapaswa kufukiza dawa hizo zinapokuwa katika kipindi wanafunzi wawapo likizo na hilo linapaswa lifanywe na wataalamu wa udhibiti wa wadudu.

Jambo linaloshauriwa ni kwamba wanafunzi wapewe elimu sahihi ya kujikinga na kunguni, inayojikita katika kuhamasisha usafi kwenye mabweni wanayolala, pia nguo zao.

Hapo inapendekezwa, mabweni shuleni na vyuoni, yanapaswa kuwa sehemu za kutunza mizigo, ili kuepusha kuhamishia kunguni vyumbani.

Pia, mambo hayo dhana yake inafika shuleni na vyuoni, kwa kutumia njia za joto, kama matumizi ya maji ya moto na kunyunyuzia sehemu ambazo kunguni huenda kujificha.

Hali kadhalika, ujumbe unawafikia walimu kwamba wanapaswa kufuatilia kwa karibu katika utekelezaji hatua zote, ili kuhakikisha unafanyika kwa usahihi zaidi.

### TAKWIMU ZA NCHI

Hadi sasa nchini kuna upungufu mkubwa wa takwimu juu ya janga la kunguni, ingawa yapo malalamiko ya wanafunzi kutoka shule na vyuo mbalimbali juu ya kusumbuliwa na wadudu hao.

Hapo kitaalamu ndiyo unatoka wito ushauri mamlaka husika kufanya tafiti zitakazobainisha ukubwa wa tatizo nchini na kupangwa mikakati madhubuti ya ufuatiliaji wa karibu, tathmini na udhibiti wa ugonjwa huo, ili kuwasaidia wanafunzi wapate muda safi wa kusoma, pasipo kusumbuliwa na wadudu aina ya kunguni.

***Maoni hayo kitaalamu yameandaliwa na Vivian Mushi, Hoseenu Palilo, Pankras Luoga, wote wahadhiri wasaidizi katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba Muhimbili (MUHAS) na wanapatikana kwa simu + 255 0757645746.***

AFYA

## MAENDELEO NA UGUMU WAKE...

# Halmashauri mpya Tunduma yaelemewa na wagonjwa, sasa vitani kupata hospitali

**Na Ibrahim Yassin, Tunduma**

CHANGAMOTO ya uhaba wa vituo vya kutoa tiba, watumishi na vitanda vya kulala wagonjwa na hasa wajawazito, imeendelea kuikumba Halmashauri mpya ya Mji Tunduma wilayani Momba, mkoani Songwe, hata kusababisha matukio ya wahusika kuhudumiwa wawili hadi watatu katika kitanda kimoja.

Kwa sasa Halmashauri ya Mji Tunduma ambayo inatokea katika iliyokuwa kata za Halmashauri za wilaya Mama Mbozi, baada ya kukua kwa kasi kutokana na Tunduma kuwa mji wa biashara mpakani na nchi jirani, ikiwemo Zambia.

Wakati mji huo ulianzia kuwa kata ya Tunduma zamani, ilikuwa na vijiji 20 inayotaabika na huduma ya vituo vya kutoa tiba, tegemeo kubwa likiwa Kituo cha Afya Tunduma. Hiyo ilifanya watu wanaotoka vijiji vya mbali kutaabika wakilazimika kupata huduma za tiba kwa waganga wa jadi, pia wajawazito wakijifungua huko.

Ni hali ya matibabu yenye historia iliyowapoteza kinamama wengi wakijifungulia kwa wakunga wa jadi na waliokuwa wakitembea umbali mrefu, kukiwepo ushuhuda wa safari kilomita 30 au zaidi athari lukuki za kiuzazi na kiafya kwa baadhi yao.

Baada ya kugawanywa mkoa wa Mbeya na kuundwa Songwe zaidi ya miaka sita iliyopita, kukaibuka maendeleo yanayobeba sura kamili ya mji wa Tunduma, lakini kukaonekana magumu mengine ghafla panaelemewa kumudu huduma ya afya, kutoka kituo chake cha afya.

Hapo ndipo kukatokea hali kituo hicho cha afya, kubeba majukumu mazito kama hospitali kamili kutokana na wengi wa wahitaji huduma, huku wahudumu wakiwa wachache na wanaelemewa kazi, Mganga Mkuu wa Halmashauri, Dk. Enock Mwambalaswa akieleza wanaojifungua ni wastani 20 hadi 25 kwa siku.

Pia, anafafanua kwamba wanajitahidi kufanikisha malengo yao kikazi, dhidi ya msongamano huo na kwa sasa wana gari moja la kubeba, pia ndilo linatumika kutembelea miradi.

### WAKAZI TUNDUMA

Edar Mwakipesile, mkazi wa Tunduma anaiambia Nipashe kwamba, katika kituo hicho cha afya, yumo katika kundi kubwa la wajawazito na amefika hapo saa moja asubuhi hadi saa saba, akiwa bado hajapatiwa huduma kutokana na uhaba wa watumishi.



Baadhi ya wajawazito wakiwa wamelala wawili kwenye kitanda kimoja baada ya kujifungua kutokana na uhaba wa vitanda uliopo kwenye kituo cha Afya Tunduma.

Hapo rai yake anaiomba Nipashe kwamba, serikali iboreshe huduma zake kwa kuongeza watumishi, vitanda, magari ya wagonjwa na majengo, ili kuondoa msongamano uliopo sasa.

Christina Fredy, mkazi wa eneo la Songea, anaeleza tatizo kubwa lililopo katika kituo hicho, ni mazingira ya kujifungua, wanaposubiri hatua hiyo wanalala kwa tahadhari kitanda kimoja, huku waliojifungua wakihofia kumlalia mtoto.

Lingine analotaja ni kuwepo gari moja na linalofanya kazi nyingi, hapo anaiomba serikali iongeze vitanda kunusuru hali yao ilivyo.

Mwenye maoni mengine ni mkazi wa mjini Tunduma, Mariam Mwazembe, anayesema amefika hapo kupima ujauzito, lakini foleni aliyoikuta anaitaja 'haijawahi kutokea', kimantiki ikimpa tabu suala la wajawazito kuchangia kitanda kutokana na hali ya msongamano.

### NENO LA UONGOZI

Alice Msufa, ni Ofisa Muuguzi Huduma ya Mama na Mtoto wa kituo hicho, anakiri wanazidiwa na idadi ya wagonjwa, kwani watumishi wako wachache, kinamama wengi wanaojifungua wanachangia kitanda, kutokana na uhaba wa huduma hiyo.

Anasema, ujenzi wa hospitali mpya utawasaidia kupunguza msongamano na hata malalamiko yaliyopo, kwani nao wanachoka wakifanya kazi, pia muda wa ziada, huku gari lao la kutoa huduma nalo likielemewa.

Hata hivyo Mganga Mkuu Dk. Mwambalaswa, anafafanua kwamba wamejipanga kukabili hali hiyo duni ndani , watumishi na miundombinu pungufu, ikiwamo kujitahidi kutembelea miradi yao vijijini.

Dk. Mwambalaswa anasema, ikama yao wahudumu wa Kituo cha Afya Tunduma jumla yao pamoja na wa kujitolea wako 57, ambapo jumla yao bado hawakidhi mahitaji ya idadi kubwa ya wahitaji huduma, ambao ni wagonjwa walio kundi kubwa la watu.

" Hebu ona leo walikuwepo wahudumu watatuambia wamewazalisha kina mama 16 na bado siku haijaisha, lakini hali hii itaisha, kwani serikali imetoa fedha kujenga vituo vya afya pamoja na hospitali kubwa," anaeleza Dk. Mwambalaswa.

Anafafanua kuwa, pamoja na kuwepo msongamano huo, bado serikali inafanya jitihada za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza hasa katika mpaka wa Tunduma na nchi jirani, ikiweka wataalamu wanaofanya kazi ya kuwapima watu wanaotoka nje ya nchi.

Dk. Mwambalaswa anaeleza kwamba, jumla ya nchi 10 zilizoko Kusini mwa Afrika (nchi za SADC) wanavuka mpaka na wameweka kifaa maalum (Scanner) kinachowapima watu 10 kwa mara moja na anayebainika kuambukizwa homa za manjano au Covid 19, anatengwa katika eneo maalumu anakopatiwa huduma zinazopatikana huko.

Ofisa Mfawidhi wa Afya katika mpaka wa Tunduma Dk. Emmanuel Kalekayo, anasema wameweka huduma hiyo kwenye jengo la pamoja kumhudumia vipimo kila mgeni anayevuka, wakiwamo madereva, kukitumika vifaa maalum vya kisasa.

Anafafanua vigezo kwamba, endapo mtu anayepimwa akiwa na nyuzi joto kufika 30 au zaidi anakuwa na dalili za Covid 19, hivyo wanamtenga na hata maiti kabla ya kuvuka, nayo hupimwa kubaini kama ina maambukizi yoyote, lengo ni kulinda usalama wa afya nchini dhidi ya wavukao mpaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Mbozi, Fillemon Magesa, anasema kuna msongamano kwenye huduma za matibabu kwenye mji wa Tunduma ambao sasa uko juu zaidi kibiashara, ukiingiza na kutoa wengi wanaofika kusaka maisha na wale wanaovuka kwenda upande wa pili wa nchi.

Magesa anaeleza, serikali imeshaliona hilo na ndiyo maana imeamua kuwekeza Sh. bilioni 7 za kujenga hospitali ya ghorofa moja ikiwa na mahitaji yote, itakayosaidia kukabili msongamano uliopo katika Kituo cha Afya Tunduma kinachoelemewa sasa.

Anafafanua kuwa, Rais Samia ameshawapa fedha, hata wakajenga vituo vya afya vya Chiwezi na Chapwa, pamoja na zahanati tatu, huku Sh. milioni 300 zikipelekwa hospitalini hapo kuongeza jengo la huduma za wagonjwa wa nje.

Magesa anafafanua, jumla kuu ya ujenzi wa vituo hivyo ni Sh. bilioni 3.2 huku serikali kuu ikitoa jumla ya Sh. Milioni 366 za kununua vifaa tiba. Hadi sasa kwa jumla, halmashauri hiyo ina hospitali moja, vituo vya afya vitano na zahanati tatu.



Wajawazito wakiwa nje ya kituo cha afya wakisubiri kupatiwa huduma ya mama na mtoto,wakitumia muda mrefu baada ya uhaba wa watumishi. **PICHA ZOTE: IBRAHIM YASSIN.**

# Nzega kutoka ndoto za maji katika tamthilia, hadi kuwa hali halisi nyumbani

**Na Mwandishi wetu**

**"Haya maji tulizoea kuyaona katika picha za tamthilia za wazungu katika maonyesho ya runinga za vibandani. Haya maji ya kuoga kama mvua, tena katika bomba tuliona ni mambo ya nchi zilizoendelea zaidi na watu wengine huko nje ya nchi na miji mikubwa tu, sio hapa kwetu."** *Bi. Ndala Kapalata, Mwenyekiti wa mtaa wa Musoma, mjini Nzega anatoa simulizi hiyo.*

Bi. Ndala anaongeza kuwa jambo hilo sasa limefutika nyumbani kwake na kwa wakazi wengine wa Nzega, anaongeza sio tu kuwa maji ya kutosha yapo, bali amefunga bomba ndani ya nyumba na alichokuwa anakiona katika runinga sasa kipo katika nyumba yake, maji ya kuoga kama mvua , shower.

Mabadiliko haya katika maisha ya wananchi ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika Sekta ya Maji, kwa kukamilika kwa mradi wa maji wa Tabora-Igunga-Nzega. Mradi huu chanzo chake cha maji ni Ziwa Victoria mkoani Mwanza, wilaya ya Misungwi katika Kijiji cha Nyang'homango, kitongoji cha Ihelele. Huduma hiyo ya maji inatolewa na kituo hicho kwa saa 23 kwa siku.

Takwimu za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (NZUWASA) zinaonyesha baada ya kukamilika kwa mradi unaotoa maji katika ziwa Victoria kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji ni asilimia 98, kabla ya mradi huo huduma ya maji ilikuwa chini ya asilimia 30.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya ya Nzega Bw. Amos Kanuda anasema kuwa awali walikuwa na shida sana ya huduma ya maji, ila kwa hivi sasa Wataalamu wa Sekta ya Maji wameondosha adha hiyo, kwa kufanya kazi kubwa ambayo imemaliza kiu ya maji kwa wananchi.

Anasema kuwa watumiaji wakuu wa huduma ya maji ni wananchi na viongozi katika mitaa wanao wajibu wa kuwajua vyema wananchi wanao hitaji kupatiwa huduma ya maji, wananchi ambao tayari wanapata huduma ya maji na kusisitiza umuhimu wa kutunza miundombinu ya miradi ya maji. Hatua hii kutaifanya huduma ya maji iwe endelevu kwa wakati wa sasa na vizazi vijavyo.

Chanzo cha maji cha Ihelele, kwa mwendo wa wastani kwa gari kutoka Nzega kipo umbali utakaochukua muda wa saa tatu nanusu kufika. Hivyo, maji wanayohudumiwa wananchi wa Nzega yametoka mbali na kazi kubwa imefanywa na Serikali katika kufanikisha hilo. Chanzo cha maji cha Ihelele kina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 80 kwa siku, hivi sasa maji yanayozalishwa ni lita milioni 54, sawa na asilimia 68, kwa siku ambazo ndizo mahitaji toshelevu kwa wananchi na maeneo mengine kama viwanda.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa kwa uwekezaji uliofanywa na Serikali, endapo idadi ya wanufaika itaongezeka, hapana shaka kuwa watahudumiwa kwa kupata huduma toshelevu ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Mkuu wa Wilaya ya Nzega Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Advera Bulimba ameiongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama kutoka katika wilaya yake, kwa ziara maalumu katika kituo cha kuzalisha maji cha Ihelele, Misungwi kuona yanapotoka maji ya Mradi mkubwa wa maji wa Tabora-Igunga-Nzega. Lengo mahsusi likiwa kujifunza.

ACP Bulimba pamoja na kamati hiyo, amejumuika na Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa kutoka Nzega kujionea kazi ya uzalishaji wa maji wanayohudumiwa wananchi wa Nzega kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Nzega (NZUWASA).



*Mkuu wa Wilaya ya Nzega Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Advera Bulimba (anayeongea) akiwa pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama kutoka katika wilaya yake, wakijionea hatua ya awali ya kutoa tope katika maji katika kituo cha kuzalisha maji cha Ihelele, Misungwi mkoani Mwanza yanapotoka maji ya Mradi mkubwa wa maji wa Tabora-Igunga-Nzega.*

Akiongea katika ziara hiyo amesisitiza kwa watendaji wa wilaya anayoiongoza kujitoa katika kuwaeleza wananchi namna bora ya kutumia huduma ya maji vizuri. Anasema hatua hii itasaidia kuepuka matumizi yasiyokuwa na lazima na kuwaepusha na gharama.

Ameweka bayana katika wilaya ya Nzega wamejipanga kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya maji karibu na makazi.

Kuendana na mabadiliko ya teknolojia, amesema kuwa yeye binafsi anatumia Dira ya malipo kabla, na inamsaidia kuangalia kiwango cha maji anachotumia, na fedha aliyolipia maji ikiisha anaongeza na kuendelea na huduma kwa wakati. Dira hiyo matumizi yake ni pamoja na mteja kujihudumia mwenyewe.

ACP Bulimba katoa heko kwa Serikali, kwa kuwatoa wananchi katika huduma za visima na sasa wanatumia maji kutoka Ziwa Victoria. "Serikali inapambana katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na maisha bora kupitia huduma ya Maji" Mkuu wa Wilaya ya Nzega ACP Bulimba anasema.

NZUWASA imefanikisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Nzega kufika asilimia 98, na huduma inapatikana kwa saa 24. Maji hayo yanatoka katika ziwa Victoria mkoani Mwanza kwa nguvu ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ambapo zaidi ya wananchi milioni moja wananufaika na maji hayo.

Viongozi kutoka Nzega wamefanya ziara hiyo ili wawe chachu katika kuwahimiza wananchi katika maeneo yao kutumia majisafi na salama ili kuepuka magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo salama. Pia, kuwa daraja katika kutoa taarifa kuhusu mivujo inayosababisha hasara kutokana na ukweli kuwa gharama za kuzalisha maji si haba, hivyo huduma ya majisafi lengo lake kuu ni kuwafikia wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (NZUWASA) Mhandisi Athumani Kilundumya anasema ziara ya kutembelea kituo cha kuzalisha maji ni moja ya darasa na ushirikishwaji kwa wadau wa mamlaka anayoiongoza.

Anafafanua kuwa lengo ni kujenga uelewa mkubwa kuhusu huduma ya maji na kutambua uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ili kufanikisha huduma ya maji kwa wananchi, na kuwa daraja katika kuhakikisha rasilimali maji na miundombinu ya miraji ya maji inalindwa.

"Ushirikishwa wa viongozi na jamii umeleta mafanikio makubwa hapa Nzega, mwaka 2021 upotevu wa maji ulikuwa zaidi ya asilimia 68, lakini hivi sasa upo chini ya asilimia 10 " Mhandisi Kilundumya anasema na kuongeza jamii imetambua hasara ya upotevu wa maji ambayo yangewahudumia zaidi, pia jamii inashiriki kutupa taarifa za mivujo ili tuokoe fedha inayopotea kwani gharama za kuzalisha maji ni kubwa.

Mhandisi Kilundumya anaweka bayana kuwa fedha iliyotolewa na Serikali katika mpango wa mwaka 2022-2023 imewapa nguvu NZUWASA na lengo ni kufikisha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kufika asilimia 100.

Salim Abdukadir, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya NZUWASA anasema amejionea jinsi maji yanavyozalishwa kwa kupitia hatua nyingi, hadi kupata maji bombani, na ukweli ni kuwa maji hayatoki ziwani na kuwekwa katika bomba moja kwa moja.

Abdukadir anasema kazi ya kuondoa tope katika maji, kupima maji na kuyatibu kupitia wataalamu wa maabara kwa saa 24 na kuyasukuma katika matenki ni moja ya kazi za msingi za kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama, na ni kazi inayotumia rasilimali fedha kubwa, pamoja na nguvu kazi ya wataalamu wanaohakikisha kila jambo linafanyika kwa kiwango.

Mkazi wa Nzega, Bw. Edson Kibachu anayefanya biashara ya kuosha magari anakubali kuwa maji wanayopata ni safi na salama na kuongeza matumizi ya teknolojia yameboresha zaidi huduma katika maeneo ya kazi.

Kibacha anafafanua matumizi ya Dira za malipo kabla yameleta mapinduzi makubwa kwani anajihudumia mwenyewe na kupima kiasi cha maji katika biashara, na hakuna haja ya msoma Dira tena.

Anaongeza kuwa maisha ya Nzega yamebadilika baada ya kupata maji ya uhakika, hapa tunajenga nyumba na ukiwa katika hatua ya msingi tu, tayari unaomba na kuwekewa huduma ya majisafi na mamlaka yetu. Hivyo, ujenzi unaenda vizuri na haupati tabu ya kupata maji.

Naye Arbogast Peter anayefanya biashara ya kuuza maji eneo la Gulioni anasema kabla ya mradi wa ziwa Victoria huduma ya maji ilikuwa ya mwendo wa kusuasua, na ilipatikana usiku zaidi. Anasema hivi sasa maji yapo mengi na yakutosha muda wote , na wateja hawasumbuki kupata huduma hiyo muhimu ya maji yanayoanzia ziwa Victoria hadi Nzega.

Maji wanayopata wananchi wa Nzega ni safi na salama. Hatua muhimu za kutibu maji zikishakamilika katika kituo cha Ihelele, maji hayo husukumwa kwa pampu kubwa kupitia bomba la chuma lenye kipenyo cha mm 900 hadi kwenye tanki kubwa katika mlima Mabale, likiwa umbali wa takriban kilomita 6.6. Tanki hilo la kuhifadhi majisafi na salama, lina uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha lita milioni thelathini na tano (35,000,000).

Kutoka tanki la Mabale, maji hutiririka kwa mserereko kuelekea kwa wateja katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Tabora na Mwanza. Mtandao wa usafirishaji maji unajumuisha mabomba makubwa yenye jumla ya urefu wa takriban km 700 na kipenyo kuanzia inchi 48 (mm 1,200) kwenye tangi la Mabale hadi inchi 8 (mm 200) kwenye matangi madogo.

Chanzo cha maji cha Ihelele kinasimamiwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama -Shinyanga. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA). Jukumu la mamlaka hii ni kuzalisha maji kutoka ziwa Victoria, kusambaza na kuuza maji hayo kwa jumla kwa mamlaka nyingine zinazohusika na usambazaji wa maji kwa wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini.

Mamlaka zinazo patiwa huduma hiyo ni pamoja na migodi na vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs). Wateja wa KASHWASA kwa upande wa mijini ni Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Shinyanga (SHUWASA), Kahama (KUWASA), Ngudu (MWAUWASA – Kanda ya Ngudu), Kishapu (KIWASA), Maganzo( MAGAWASA), Tabora (TUWASA), Nzega (NZUWASA) na Igunga (IGUWASA).

Kwa upande wa vijijini, KASHWASA ina jumla ya wateja 87, ambao ni Vyombo vya Watoa Huduma za Maji Ngazi ya Jamii vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Kwimba, Shinyanga, Msalala, Kishapu, Maswa, Nzega, Igunga na Uyui. Pia, Mamlaka ina Wateja watatu wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini katika maeneo ya Mwadui na Mwakitolyo. Wateja hao ni Kampuni ya Williamson Diamonds Limited-WDL, ZEMD - Mwakitolyo na Zube & Jonta Investment.

168861

AFYA

# Mitandao jamii ilivyo chanzo kikubwa madhara usalama wa akili kwa umma




Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Magonjwa ya Akili Mirembe, Dk. Erasmus Mndeme, akitoa taarifa ya matatizo yanayochangia magonjwa hayo, katika halfa mojawapo ya maadhimisho ya Siku ya Afya Duniani, mjini Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Lucia Wilbert, SJMC**

KUNA swali huwa linaulizwa katika jamii, ikiwa msingi umeharibika nani atasimama kuujenga? Zama hizo, kulikuwa kunahojiwa na kushangaa, inawezekanaje mtu akajitoa uhai wake na kuwaacha wapendwa wake nyuma, pia taifa lake ambalo kesho atatakiwa kulisimamia liweze kuendelea?

Huwa wahusika wanatoa maoni yao, kuhusu kilichowasukuma kufikia hatua hiyo na wapo wanaotoa sababu zao kufikia dhamira hiyo .

Hata hivyo, katika taarifa za majumuisho na hata ripoti rasmi, huwa kuna vyanzo vyake hubainika, kukiwapo sababu zilizozoeleka na kuaminika, suala la uhusiano wa kimapenzi unapoingia kasoro kwa vigezo kama kusalitiana.

Hapo huwa kunaendana na kushuhudiwa shida ya kisaikolojia, ambayo ndiyo inakaribisha madhara na majanga kama vile mtu kujiua au kuua, ama kudhuru au kujidhuru. Pia, kuna kuibuka matatizio ya akili na adha ambazo katika sura tofauti zinahusiana na mitandao jamii.

Kumekuwapo mashauri mengi, ya kwenye mitandao ya jamii yanagusa mioyo ya wahusika kuhusu sintofahamu inayohusiana na mapenzi. Mfano wa mojawapo ukisoma "Natamani hata nife niachane na hii Dunia,"; "nimechoka kuishi"; " nahisi kuchanganyikiwa"; " najihisi kufa"; "natamani nipumzike kwa amani".

**JICHO LA WHO**

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema katika kila wastani wa vifo 100 na jumla duniani kwa mwaka jana duniani walijiua zaidi ya watu 700,000.

Pia kunaelezwa wastani huo ukiwekwa katika idadi ya kila watu 100,000, bara Afrika linaongoza kwa wanaojiua wakiwa asilimia 11.2 (watu 11,200); ikifuatiwa na Ulaya, asilimia 10.5 (watu 10,500); Asia Mashariki asilimia 10.2 (watu 10,200); na Kusini mwa Mediterrean ambako ndiko pana kiwango kidogo sana, kwa asilimia 6.4 (watu 6,400).

Hata hivyo, taarifa ya faraja kutoka WHO ni kwamba, hali imepungua kwa wastani wa asilimia 36 katika kipindi kati ya mwaka 2000 hadi 2019.

Walakini kinachoshuhudiwa ni kwamba, bado kwenye jamii kunaonekana kushindwa usimamazi wa kuhakikisha watu wa kada hiyo kisaikolojia wanasaidiwa kufikia kuepuka madhila ya madhara hayo, hata wasichanganyikiwe na kujitoa uhai, sehemu kubwa ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 19.

**WADAU AFYA**

Charles Kalungu ni mtaalamu wa afya ya akili, kutoka asasi ya Psychezone International, anasema matatizo ya akili nchini yapo makubwa, matatizo yakichangia kuwapo hali hiyo kwa wengi.

"Magonjwa ya akili ni tatizo ambalo hutokea katika ubongo kwa kumfanya mtu kuwa na hisia na matendo tofauti na yanayotarajiwa na jamii na kushindwa kukabiliana na changamoto za maisha," anafafanua.

Anaeleza namna kada hiyo iliyo katika majonzi, wengi huamua kutumia huduma ya simu kujifunza, kujifariji, kuona na pale wanaposhindwa kufikia lengo, ndio kunashuhudiwa azma ya kujikatiza uhai au wengine wanadhurika akili wakichanganyikiwa.

Kalungu anaelezea: "Kuna baadhi ya watu wanatawaliwa na hofu na mashaka kutokana na mazingira au malezi aliyokulia, kiasi kwamba hawawezi kuchangamana na watu wengine. Hata katika maisha halisi na hata kwenye mitandao ya kijamii na ndiyo kundi pia linaloathirika kwa kiasi kikubwa."

"Wanapofunuliwa wazi kwenye mitandao ya kijamii kwa namna wasiyopenda, inapelekea kuathirika," anafafanua na kuongeza: "Baadhi ya waathirika hukosa cha kufanya na kujenga ngome na uhitaji wao kwenye mitandao na wakati mwingine kila saa hujihisi kuna mtu amemtumia ujumbe."

"Anapofungua Instagram, Facebook, Twitter au WhatsApp bila ya kukuta ujumbe anaoufikiria, inapelekea changamoto," anaeleza.

Humphrey Msangi, mwanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, ni mmiliki wa kurasa mbalimbali katika mitandao ya kijamii, anafafanua uzoefu wake kuhusu hilo, akisema: "Hili limekuwa tatizo na changamoto kubwa sana.

"Bado jamii imelala, wa haijaona kuwa kuna shida kutokana na watu wengi wanapoweka picha zao mtandaoni, hugeuka kuwa fimbo ya kumchapia yeye (muweka picha) na kumchafua kwa namna ya kumkashifu.

Hata wanapoomba kusaidiwa kiushauri, inakuwa ni machungu, kwani hakuna mwenye mchango chanya ila matusi, kejeli na dhihaka"

Pia, anazungumzia tatizo la watu wengi kuwa waraibu wa mitandao ya kijamii na pale wanapokosa hela ya kununulia bando, ili kumuwezesha kuingia kwenye mitandao ya kijamii humfanya kuathirika sana kiakili, kwa hofu ya kupitwa au kukosa kujua kinachoendelea.

Anasema, ni hulka inayowafanya pale wanapokosa pesa za kunulia bando, huwa wanatafuta mbadala ambao si halali na ndio mwanzo wa shida kijamii inapochukua nafasi.

Poa, anasema pale mitandao ikirahisisha mawasiliano na taarifa zake, inafungua milango ya madhila na inakuwa hakuna siri za umma, bali ni unyanyasaji wa kijamii

# Ushindi tiba kwa watoto 10,000 vifundo miguu

**Na Yasmine Protace**

VIFUNDO miguu, ni maradhi ambayo mtoto anazaliwa akiwa na miguu imepinda, hata kumkosesha unyayo.

Inaelezwa kuwa baadhi ya wazazi wanaojifungua watoto wenye ulemavu huo huwaficha watoto wao, athari zake huishia kuwapa watoto hao ulemavu wa kudumu.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya CCBRT,iliyopo Jijini Dar es Salaam, Dk. Cyprian Nyomoka anasema kuna jumla ya watoto 800,000 duniani wanaozaliwa kila mwaka na tatizo hilo la 'miguu vifundo.'

Nchini Tanzania, Dk. Nyomoka anatoa wastani wa takwimu wanakaribia 300,000, kauli anayotoa katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Miguu Kifundo, ambayo kila mwaka duniani hufanyika Juni 3.

Anasema,ugumu walio nao ni kwamba baadhi ya wazazi hawafiki katika vituo vya tiba kama vile CCBRT kuwapeleka watoto kupatiwa matibabu.

Dk. Nyomoka anasema, matibabu yanachukuwa miaka hata mitano kumuwezesha mtoto kurudia uhalisi wa miguu inavyotakiwa kuwa, lakini muhimu kwanza ni kwa mzazi afike katika kliniki kila anapopangiwa na endapo asipohudumiwa vizuri mtoto hawezi kupona.

"Mtoto aletwe mapema CCBRT ili aweze kufanyiwa matibabu aweze kupona na kama anacheleweshwa kupatiwa matibabu, uponaji wake unakuwa mgumu," anasema.

Pia, anaishukuru asasi anayoitaja Miracoseet, kwa kuwafadhili fedha za kutoa huduma tajwa bure kwa watoto wanaofika kliniki kupata matibabu ya miguu kifundo.

Hata hivyo, ana angalizo kwamba hali ya uchumi kwa baadhi ya wazazi inakuwa changamoto, wazazi wanashindwa kupata nauli za kutoka maeneo waliko, ili kuweza kufika CCBRT kwa ajili ya matibabu.

Kwa mujibu wa Dk. Nyomoka, CCBRT ilianza kutoa matibabu ya miguu kifundo tangu mwaka 2001 na

kwa mwaka mzima watoto zaidi 100,00 hufanyiwa matibabu vifundo.

Anasema, kila mwaka watoto wagonjwa wapya zaidi ya 300 hufika kupata matibabu. Anaendelea: "Watoto wakichelewa kupata matibabu vifundo navyo huzidi kukomaa."

Anasema, baadhi ya familia zina changamoto ya kifedha, wanashindwa kurudi kuendelea na matibabu na badala yake mtoto anabaki kwenye ulemavu wa kudumu.

Dk.Frank Yalebi kutoka CCBRT, anasema watoto kuzaliwa na vifundo, inaweza kuanzia mama mjamzito kupata mtoto mwenye kifundo, inatokana na mtoto kukunja miguu pale anapokuwa tumboni.

Anasema, wajawazito hawatakiwi kutumia kilevi na hawatakiwi kutumia dawa ambazo hawajapewa na mtaalamu wa afya, kwani inaweza kuwa chanzo, huku akitaja

watoto wa kiume ni miongono mwa wanaoathirika na vifundo zaidi.

Mwajuma Ally, mzazi ambaye mtoto wake anaendelea kupata matibabu, anasema kuwa alimzaa mtoto akiwa na tatizo katika mguu mmoja,baada ya kupata taarifa za CCBRT, aliwahi kumpeleka mtoto wake na sasa anaendelea vizuri.

# Polisi wamulika madereva bajaj

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martine Otieno, amesema Jeshi la Polisi litachukua hatua kali dhidi ya madereva bajaj watakaopakia abiria tofauti na idadi inayotakiwa.

Kauli ya Kamanda Otieno inakuja siku chache baada ya ajali ya gari na bajaj kutokea maeneo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na kusababisha vifo vya wanafunzi watatu na dereva bajaj.

Ajali hiyo iliyokatiza maisha ya vijana hao, ilitokea maeneo ya UDOM baada ya gari aina ya RAV4 kugongana uso kwa uso na bajaj na kusababisha vifo hivyo, bajaj ikiwa imebeba abiria tisa tofauti na idadi inayotakiwa.

Majeruhi wa ajali hiyo wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa iliyoko jijini Dodoma kwa ajili ya matibabu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda Otieno alisema madereva wa bajaj wanapaswa kuzingatia taratibu na sheria za usalama barabarani ili kujilinda wao na abiria wanaopanda na chombo husika cha usafiri.

Alisema madereva watakaobainika wamepakia abiria zaidi ya idadi ya wanaotakiwa, jeshi hilo litawachukulia hatua za kisheria ili kuhakikisha linalinda usalama wa raia.

"Ninaomba madereva wazingatie taratibu na sheria za usalama barabarani. Bajaj sio Noah mpaka upakie watu zaidi ya sita, mnachotakiwa ni kupakia abiria watatu na dereva," aliagiza Kamanda Otieno.

Alisema Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wananchi ili watambue sheria za barabarani zinasemaje kuhusu vyombo vya usafiri barabarani.

Kadhalika, alisema wataendelea kutoa elimu kwa madereva wa vyombo hivyo vya moto ili kuhakikisha wanaepusha ajali zinazojitokeza kutokana na uzembe unaofanywa na madereva.

Alitoa wito kwa wananchi kuwa makini na vyombo vya usafiri barabarani na kuongeza kuwa wasikubali kupanda chombo cha usafiri kama kimezidi idadi ya abiria wanaotakiwa kuwamo ndani.

**Alisema madereva watakaobainika wamepakia abiria zaidi ya idadi ya wanaotakiwa, jeshi hilo litawachukulia hatua za kisheria ili kuhakikisha linalinda usalama wa raia**

# Serikali yafanya mapitio mitaala elimu ya ufundi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali inafanya mapitio ya mitaala ya elimu inayotolewa kwenye vyuo vya ufundi ili kuwa na wahitimu wenye ujuzi unaohitajika katika soko la ajira nchini.

Katambi alibainisha hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifungua kongamano la kwanza la elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET).

Alisema serikali inafanya mapitio ya mitaala ya elimu ya mafunzo ya ufundi nchini ili iendane na mahitaji ya soko la ajira nchini hali itayosaidia kupunguza kuajiri watu kutoka nje.

Katambi alisema mapitio hayo yatawezesha taifa kupata wahitimu wenye ujuzi ambao unahitajika katika soko la ajira nchini tofauti na ilivyo sasa.

"Lakini pia hali hii itasaidia kufungua sekta binafsi na kuongeza ajira nchini, huwezi kukua kiuchumi wakati hujafungua ajira, mikakati yetu ya serikali kwa sasa ni kuhakikisha kuwa tunafungua ajira. Rais anaitumia sekta ya uwekezaji kukabili tatizo la ajira nchini na kupandisha 'happiness Index'," alisema Katambi.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Adolf Lutayunga, alisema lengo la kongamano hilo ni kujadili mustakabali wa mafunzo ya ufundi nchini.

Alisema lengo ni kujenga vijana wanaoweza kuajirika kupitia mafunzo ya ufundi yanayotolewa katika vyuo nchini.

"Mada katika kongamano hili zitalenga katika kutafuta namna ambavyo tunakuza ujuzi katika vyuo vyetu vya ufundi ili kuwa na wahitimu ambao wana ujuzi unaohitajika katika soko la ajira nchini.

"Hapa tumekutana walimu, wataalamu kutoka vyuo vya ufundi, waajiri pamoja na wadau wengine wa maendeleo ili kuona hichi ambacho hivi sasa kinafundishwa katika vyuo vyetu kama ndicho kinahitajika katika soko la ajira," alisema.

Kadhalika, alisema kongamano hilo linahusu kukuza na kurasimia ujuzi ili kuongeza wigo wa vijana wenye maarifa na mitaji.

"Pia tumewaalika watu mbalimbali kutoka katika mataifa mengine ndani ya Afrika na nje ambao watatusaidia kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya urasimishaji ujuzi kwa vijana wanaokidhi soko la ajira," alisema.

Vilevile, alisema kuwa kutokana na waajiri pamoja na vyuo vya ufundi kila mmoja kufanya kazi bila kumshirikisha mwenzake, kumekuwa chanzo kuzalishwa kwa wahitimu ambao hawakidhi mahitaji ya soko la ajira.

"Katika kongamano hili waajiri pia watapata fursa ya kuzungumza na watu wa vyuo vya ufundi ili kupata kitu wanachokihitaji katika soko la ajira," alisema Lutayunga.




Meneja wa Mazingira na Usalama wa Tanzania Breweries Ltd (TBL), Revocatus Rutakwa (kushoto) na Msimamizi wa Masuala ya Mazingira wa TBL, Coleta Momburi, wakionyesha tuzo na cheti cha pongezi walivyopokea kutoka ofisi ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutambua mchango wa kiwanda cha TBL katika jitihada na shughuli za utunzaji mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yaanika mikakati ya kukabili uharibifu wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, amebainisha mikakati ya baraza hilo katika kukabiliana na tatizo za uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza hivi karibuni jijini hapa kwenye maonyesho Wiki ya Mazingira, Dk. Gwamaka alisema hali ya mazingira nchini siyo nzuri, hivyo wameweka mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi, kusimamia sheria na kanuni ikiwamo kuwapa adhabu kali wale wanaofanya vitendo vya uharibifu wa mazingira.

"Mkakati wa kuelimisha umma unalenga wananchi kutii sheria bila shuruti na hili linakuja kwa kutoa elimu mtu akikata miti ahakikishe anapanda miti, pia suala la taka ngumu na kelele limekuwa shida," alisema.

Dk.Gwamaka alisema sababu za uharibifu wa mazingira zinajumuisha ongezeko la watu, misitu kuvamiwa na shughuli za binadamu kuendelea katika maeneo ya vyanzo vya maji.

"Sehemu ya vyanzo vya maji imevamiwa, yale maeneo yaliyotengwa mita 60 wameshindwa kuyalinda na baadhi ya watu wanatumia kilimo cha umwagiliaji kutoka mtoni.

"Ukienda Kigoma, Katavi, Mtwara kuna shughuli kubwa za kibinadamu zinaendelea, hali siyo nzuri kwa upande wa rasilimali za misitu.

"Kumekuwa na ongezeko la mmomonyoka wa udongo, hivyo mito yetu kujaa udogo na katika milima ambayo ilikuwa ni hifadhi, sehemu kubwa imevamia Mbeya, Uruguru hata kule Usambaani maeneo makubwa yamevamiwa. Mvua ikinyesha hakuna utulivu wa maji, hivyo kumekuwa na mafuriko," alifafanua.

Aliongeza: "Tumekuwa tukitoa elimu kwa viongozi wa dini na kwa wamiliki wa kumbi za starehe, maeneo mengine utupaji wa taka ngumu zote hizo ni changamoto."

Mkurugenzi huyo alizitaja hatua ambazo wamechukua wakizichukua ni pamoja na kuwapiga faini wale wenye makosa pamoja na kuhakikisha mazingira yanakuwa safi.



# Watoto wenye ulemavu kupatiwa msaada kiafya

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

ZAIDI ya watoto 100 wa kike wenye ulemavu kutoka shule nane za msingi na sekondari jijini Mbeya, wanatarajiwa kupatiwa taulo za kike kutoka kwenye shirika lisilokuwa la kiserikali la Empower Youth Prosperity (EYP) chini ya mradi wa afya wa hedhi na usafi.

Mradi huo unalenga kumsaidia mtoto wa kike kupata taulo za kike ili asome kwa utulivu hata kama watakuwa kwenye siku za hedhi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa shirika hilo, Ipyana Mwakyusa, wanajikita katika kutoa elimu kwa jamii hususani wazazi na walezi ili kuhakikisha suala la ununuzi wa taulo za kike linakuwa sehemu ya bajeti zao wakati wa kupanga bajeti za familia.

Alisema wazazi au walezi kwa kufanya hivyo, watamsaidia mtoto wa kike pindi anapokuwa kwenye siku zake, kujiamini na kusoma kwa utulivu kwa kuwa tayari atakuwa amejisitiri.

"Tulianzisha mradi huu wa hedhi salama na usafi kwa lengo la kuwajengea ujasiri watoto wa kike hususani walio katika umri balehe kuona kwamba suala la kuvunja ungo ni sehemu ya ukuaji na kwamba hedhi haiwezi kuwa kikwazo katika kutimizi ndoto zao za kupata elimu.

"Hivyo, shirika letu la EYP kwa kushirikiana na wadau mbalimbali linaendelea kutoa taulo za kike kwa mabinti shuleni ambapo katika harambee tuliyoifanya hivi karibuni, tulipata taulo za kike za kuwasaidia mabinti 1,000," alisema Mwakyusa.

Aliongeza kuwa shirika hilo lina lengo pia la kuwawezesha mabinti wanaoishi katika mazingira magumu kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama vile taulo hizo zinazoweza kutumika tena baada ya matumizi ya awali.

Alisema EYP inaamini kwamba suala la hedhi ni mtambuka, hivyo wanaume nao wanashirikishwa ili kufanikisha safari ya binti au mwanamke anapokuwa kwenye siku zake kabla na baada ili asikwamishwe wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kielimu au kiutumishi.

"Kulingana na utafiti uliofanywa na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na UNFPA chini ya programu ya mpango wa kuongeza kasi ya afya ya uzazi, haki na uwezeshaji wasichana nchini mwaka 2018, inaonyesha asilimia 17 ya wanafunzi wa kike hukosa masomo kipindi cha hedhi," alisema Mwakyusa.

Aliongeza kuwa EYP itaendelea kushiriki kikamilifu kumsaidia mtoto wa kike mkoani Mbeya kusoma kwa utulivu na kuweza kutimiza ndoto yake ya kupata elimu bila kikwazo chochote pindi anapokuwa hedhi kwa kupatiwa taulo hizo.




Mwanahabari Mwandamizi na Mwezeshaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanahabari, Jesse Kwayu, akitoa ufafanuzi kuhusu Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari nchini ya Mwaka 2016, wakati wa warsha ilioandaliwa na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika tawi la Tanzania (MISA – Tanzania), jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Walaani mauaji, ulawiti na ubakaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa kutetea haki za binadamu na kupinga vitendo vya ukatili nchini wamelaani vitendo vya mauaji, ulawiti na ubakaji vinavyoripotiwa maeneo mbalimbali nchini kwa kuwa vimekuwa vikisababisha maumivu makubwa kwenye mioyo ya watu.

Mkurugenzi wa Shirika la kusaidia Wanawake na Watoto nchini (WOCWELES), Mary Mushi, alisema jana kuwa watoto na wanawake ndiyo waathirika wakubwa wa vitendo hivi.

Alisema kuwa ili kukabiliana na vitendo hivyo, viongozi wa vijiji, mitaa na kata wanapaswa kuendelea kutoa elimu juu ya madhara yatokanayo na vitendo vya ukatili wa kijinsia na kwamba itasaidia kupunguza vitendo hivyo kushamiri katika jamii.

Alisema sambamba na kutolewa elimu kwa jamii, pia kunapaswa kuwapo wataalamu wa saikolojia katika ofisi za kata ambao watakuwa na jukumu ya kutoa ushauri kwa waathirika wa vitendo vya ukatili hususani wanandoa ili kuwaepusha na vitendo vya kujichukulia sheria mikononi ikiwamo kuuana.

Kuhusu watoto, alisema madawati ya jinsia na maofisa ustawi wazungukie maeneo mbalimbali kuongea na watoto hususani walioko shuleni kujua madhila wanayokumbana nayo shuleni au nyumbani na kujua namna kuwasaidia watoto hao ili kujiepusha na vitendo vya ulawiti na ubakaji au kufahamu ni mamlaka gani zinazoshughulika na vitendo hivyo.

"Migogoro ya wanandoa imekuwa chanzo kikubwa cha vitendo vya ukatili ikiwamo mauaji yanayoripotiwa nchini, tunahitaji wanasaikolojia kutusaidia ili kuokoa uhai wa watu kwa watoto kuna tatizo la malezi kwa wazazi maana kuna baadhi hawako karibu kabisa na watoto wao.

"Hivyo, ni ngumu kujua matatizo wanayokumbana nayo sisi kama wadau wa haki za wanawake na watoto tunaendelea kuweka nguvu kwenye eneo hilo ili kuokoa kizazi chetu na kuwasaidia kuepukana na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu," alisema Mushi.

# Waandishi wapewa mbinu kukabili vikwazo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAANDISHI wa habari mkoani Mbeya wamehamishwa kuungana kupitia Chama cha Wanahabari mkoani humo (MBPC) ili kujadili vikwazo na mahitaji mbalimbali ya vifungu vya sheria vilivyoko kwenye sheria mpya ya huduma ya vyombo vya habari nchini ya mwaka 2016.

Mwanahabari mwandamizi nchini, Jesse Kwayu, alitoa rai hiyo jana alipokuwa mwezeshaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanahabari wa Mkoa wa Mbeya, kutambua sheria mbalimbali za huduma ya vyombo vya habari nchini pamoja na wajibu wa wanatasnia kutimiza wajibu wao yaliyoandaliwa na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-TAN).

Alisema MISA-TAN imeendelea kuwajengea uwezo wanahabari mbalimbali nchini kufahamu sheria mbalimbali za habari na kuzichambua kwa pamoja na kuainisha mahitaji yao ili yafikishwe kwenye Wizara ya Habari kama maelekezo ya Waziri Nape Nnauye alivyoagiza kwamba anahitaji maoni ya wanahabari kwenye sheria mpya ya vyombo vya habari nchini.

Kutokana na hilo, alisema Chama cha Wanahabari Mkoa wa Mbeya (MBPC) kianze mara moja kuratibu maoni hayo na kwamba yakishachakatwa yanapelekwa kwa viongozi ambao watawasilisha maoni hayo kwa kuzingatia mahitaji ya wanahabari hao.

"Waziri Nape alitoa maelekezo kwamba hadi kufikia mwezi Septemba mwaka huu maoni na mapendekezo juu ya sheria mpya ya huduma ya vyombo vya habari nchini awe ameyapata ili aanze kuyapitia na kuyachakata, hivyo ni fursa kwenye wanahabari kupitia umoja wetu wa Press Club kuainisha mahitaji yenu ili yafikishwe sehemu husika," alisema Kwayu.

Mwenyekiti wa MBPC, Nerbart Msokwa alisema jambo hilo litafanyika kwa haraka na kwamba wanahabari wote wa Mkoa wa Mbeya watashirikishwa ili kutoa mapendekezo na maoni kuhusu marekebisho ya sheria hiyo.

Aliishukuru MISA-TAN kwa kuandaa warsha ya kuwajengea uwezo wanahabari kuzitambua sheria mbalimbali, uzuri na upungufu wake na kuwaomba kuwapatia elimu hiyo mara kwa mara ili kupata uelewa na kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia weledi, sheria na kanuni za kihabari.



# Serikali yageukia afya ya bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema afya ya bahari imeharibika na kuhatarisha ustawi wa maisha ya watu ambao kwa kiasi kikubwa wanaitegemea.

Kutokana na hilo, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amesema elimu ya matumizi sahihi ya bahari imeanza kutolewa kwa maslahi ya vizazi vya sasa na baadaye.

Waziri Makame aliyasema hayo jana mjini Zanzibar wakati wa maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani ambayo kila mwaka huadhimishwa Juni 8.

Maadhimisho hayo ambayo yamebebwa na kaulimbiu ya 'Uhuishaji: Hatua ya Pamoja kwa Ajili ya Bahari' yalihudhuriwa pia na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Soraga na wadau wengine wakiwamo mabalozi wa mazingira.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Waziri Makame alisema wizara yake ndiyo yenye jukumu hilo na imeanza kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya bahari.

"Mazingira ya bahari yanasaidia uvuvi, ufugaji wa samaki, biashara, uvunaji wa chumvi, kilimo cha mwani na utalii," alisema.

Kiongozi huyo alisema bahari kwa muda mrefu imeendelea kuwa muhimu kwa watu wa Zanzibar, hivyo utunzaji wake unasaidia utekelezaji wa dhana ya uchumi wa buluu.

Alisema hatua hiyo imelenga kukabiliana na matatizo ya uvuvi haramu na uvamizi wa maeneo ya uvuvi baharini kutoka nchi jirani.

Waziri huyo alizitaka taasisi za umma na binafsi kuongeza ushirikiano katika kuhiifadhi ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya uhifadhi uhamasishaji wa jamii kuhusu matumizi bora ya bahari.

"Tutapohifadhi bahari, tutavilinda viumbe hai vya baharini ikiwamo viumbe adimu kama vile kasa na pomboo na uhuishaji wa bahari ndiyo msingi mkuu katika kufikia dhana ya uchumi wa buluu," alisisitiza.

Balozi wa Sycheles nchini, Maryvonne Pool, alisema kuwa sera ya uchumi wa buluu nchini kwake ilianza zamani lakini elimu inahitajika katika kuelimisha jamii katika utunzaji wa mazingira ya bahari ili kupata maendeleo kupitia sera hiyo.

Alisema mafanikio waliyoyapata yametokana na elimu iliyotolewa kwa umma ambapo uliaminishwa kuwa ni dhambi kutumia zana za uvuvi zikiwamo nyavu zenye macho madogo ambazo Zanzibar zinatumiwa na wavuvi.

"Sisi (Sycheles) kabla ya kuanza utalii na uchumi wa buluu, ilikuwa ukifungua vyombo vya habari unasikia elimu wa uchumi wa buluu na utunzaji wa bahari hivyo elimu ni muhimu katika kutunza mazingira," alisema.

Meneja Mradi wa Uhifadhi wa Kisiwa cha Chumbe (CHICOP), Benjamin Taylor, alisema kuwa kupitia mradi wa uhifadhi wa kisiwa hicho kumeiwezesha Zanzibar kupata tuzo mbili za kimataifa kuhusiana na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

"Kupitia mradi huu, makundi mbalimbali yameelimishwa na kusababisha kuwapo kwa ongezeko la mapato ya baharini lakini kama nchi imeshinda tuzo ya Kanda ya Kusini ya dunia na tuzo ya kimataifa kwenye masuala ya uhifadhi wa mazingira," alisema.

## Spika awabana mawaziri kutatua tatizo uhaba maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, amewataka watendaji wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili wananchi katika majimbo ya uchaguzi likiwamo tatizo la uhaba wa maji.

Alitoa maagizo hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi baada ya wajumbe wake kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Maulid alisema wizara ya maji imeongoza kwa wajumbe wengi wapatao 60 kuchangia na aliruhusu hilo kutokana na matatizo makubwa ya maji safi na salama.


Alisema wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji ambapo mifumo mingi ni chakavu.

Spika huyo aliitaka Wizara ya Maji kufuatilia kwa karibu fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali ambazo ni nyingi na kama zitatumika vizuri matatizo ya majisafi na salama yanaweza kuondoka.

Mapema akijibu hoja za wajumbe, Waziri wa Wizara hiyo, Shaibu Kaduwara alisema wamejipanga kuzitumia vizuri Sh. bilioni 34.2 ambazo ni fedha za UVIKO-19 kuyapatia ufumbuzi matatizo ya majisafi na salama Unguja na Pemba.

Alisema Serikali ya Zanzibar inatekeleza mradi mkubwa wa uhuwishaji na uimarishaji wa miundombinu ya majisafi na salama unaotekelezwa na Benki ya Exim kutoka India ambao utaiwezeshaji mamlaka ya Majisafi na Salama kutumia vizuri nishati hiyo.

"Mamlaka ya Majisafi na Salama ipo katika hatua za mwisho za wateja wake wote kutumia mita zitakazoweza kujua matumizi halisi ya nishati ya maji kwa wateja wake," alisema.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na madaktari bingwa kutoka Jamhuri ya Watu wa China, wanaotoa huduma za afya katika Hospitali za Unguja na Pemba, walipofika Ikulu jijini Zanzibar juzi, kwa ajili ya mazungumzo na kukabidhi vifaa tiba na dawa mbalimbali. **PICHA: IKULU**

## Dk. Mwinyi asifu mchango wa China kuimarisha afya

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Serikali ya China kwa mchango wake wa kuunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar wakati wa mazungumzo baina yake na timu ya madaktari bingwa kutoka Jimbo la Jiangsu, China ambao wanatoa huduma katika hospitali za Zanzibar.

Katika mazungumzo hayo, Rais Mwinyi alisema kwa kipindi kirefu Serikali ya China imekuwa ikiisaidia Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya kwa kutoa dawa, vifaa na madaktari ambao wamekuwa wakifika visiwani humo kila mwaka.

Rais Mwinyi aliishukuru timu ya madaktari hao wapatao 21 ambao wanatoa huduma ya afya na kuwaeleza kuwa huduma wanazozitoa inasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uhaba wa madaktari bingwa, dawa na vifaa tiba katika hospitali za Zanzibar.

"Ninawapongeza kwa kutoa huduma za afya zikiwamo zile za upasuaji wa kutumia teknolojia ya kisasa ambazo zimeweza kusaidia kuimarika kwa huduma za afya nchini," alisema.

Pia Rais huyo alipongeza juhudi zinazochukuliwa na timu hiyo ya kuwasomesha madaktari wazalendo ambao wanatoa huduma za afya katika hospitali kadhaa za Unguja na Pemba.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema dawa pamoja na vifaa tiba vilivyotolewa vina gharama ya zaidi ya Sh. milioni 300.

Kiongozi wa timu ya wataalamu hao, Dk. Qu Li Shuai alimweleza Rais Mwinyi kuwa wapo 21 na kati yake, 12 wanatoa huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na tisa Hospitali ya Abdalla Mzee kisiwani Pemba.

Akifafanua kuhusu misaada hiyo waliyotoa, Song Jianqing alisema kwao ni mwendelezo wa utamaduni wa uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati ya Zanzibar na China ambao umewekwa na waasisi wa nchi mbili hizo.

Jianqing alisema walifika visiwani humo mwezi Septemba mwaka jana na tayari wameshatoa matibabu kwa zaidi ya wananchi 50,000.

Alisema wamewafanyia upasuaji zaidi ya wagonjwa 6,000 katika Hospitali za Mnazi Mmoja, Abdalla Mzee na Kivunge kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo ni ya kwanza kufanyika Tanzania.

"Tumefanya upasuaji zikiwamo za koo, masikio, macho, uchunguzi wa mfumo wa njia ya chakula na nyinginezo ambazo hapo mwanzo huduma hizi zilikuwa zikipatikana Tanzania Bara," alisema.

Pia alisema wameanzisha mafunzo kwa madaktari wazalendo hatua ambayo itazidi kuimarisha sekta ya afya, Zanzibar.

Kuhusu vifaa walivyokabidhi, alivitaja baadhi kuwa ni ECG defibrillator, potable echocardiography machines, probes, Trocar kwa ajili ya upasuaji wa laparoscopic, video ya laryngoscope, electric negative pressure suction devices, oxygen generators, multifunctional monitors, mesh, surgecal sutures.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DENIS BRAYSON MUSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1088-0089** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondary ya **TUMBI** mwaka **2015**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Polisi taarifa KBA/RB/2454/2022**

## TANGAZO



KUANZIA TARAHE **26/5/2022** SITATUMIA TENA JINA LA ZAMANI LA **FATUMA ABDALLAH THABIT** BADALA YAKE NITATUMIA JINA LA SASA **FATUMA ELIASA THABIT** LINALOONEKANE KATIKA VYETI VYANGU VINGINE.

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDWIN LEO MPAHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index **namba S.111/505** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **ITAGA SEMINARY mwaka 1981**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa MO/PS/BI/35/VOL/XXX/221**

**JAMHURI YA MUUNGANO**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe**
**Kituo cha njombe mjini**
**Mkoa wa njombe**
**Usimamizi wa mirathi na.33/2022**
**Daudi Aloyce Sapula....................marehemu**
**Justine Aloyce Sapula................mwombaji**

### TAARIFA KWA WADAI

*(kanuni ya 9(1) ya nyongeza ya V ya sheria ya mahakimu wa mahakama sura ya II rejeo la 2019)*

**TAARIFA** inatolewa hapa kwa watu wote wanaodai kuwa na madai yanayohusika na mali za marehemu mtajwa hapo juu Daudi Aloyce Sapula aliyefia hospitali ya kanda mbeya tarehe **25/04/2022** na mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo mimi Justine Aloyce Sapula siku ya tarehe 07 mwezi juni mwaka 2022,hapo sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia sanduku langu barua 54 njombe au namba ya simu 0737387028 au kuniletea kwa binafsi ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoisha nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili nikizingatia tu madai ambayo kwayo nitakuwa nimearifiwa.

Justine Aloyce Sapula

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 63 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**OMARY HATIBU MASEMULO**

**By 1. BIBIANA GASPARY MGWEDE**
**2. ..........................................**

**All persons** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **22 day of....06 .........2022**
**Dated at MOROGORO this 08 day of 06 .........2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KADI YA BAJAJI

**PENDO EDWARD MLIGO**
ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **BAJAJI(TVS-BLUE)** yenye namba za usajili **MC 247BZC**
Chassis namba:
**MD6M14PA6J4D14150**
Injini namba : **AKA4DJ4017928**
Chasis Namba:
**TYAFE659FGDS1795**
Kadi Namba : **7795032**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
**Taarifa ya polisi RB namba MKB/RB/108/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha KIHONDA Mkoa Wa MOROGORO**
**Shauri la madai / ndoa na 28/2022**
**Jina la Mdai SWALEHE ABDALLA MHANDO**
**Jina la Mdaiwa AISHA BUYUNI JAHAZI**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

*(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za madai katika mahakama za mwanzo)*

**Kwa AISHA BUYUNI JAHAZI**
**DAR ES SALAM, 0717-345310**

Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba ( Eleza hapo habari za mdai ) KUJA KUSIKILIZA SHAURI LA MADAI YA TALAKA NO 28/2022 ILIYOFUNGULIWA ZIDI YAKO KATIKA MAHAKAMA TAJWA HAPO JUU.
Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakam hii tarehe 09 mwezi 06 mwaka 2022 saa2.30 Asubuhi/ mchana kwa mujibu wa madai haya vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juuu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakamani inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo....
**Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa Mahakam leo tarehe 02/06/2022.**

**HAKIMU**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 56 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late**
**ERNEST ELINAZI VIANGA**

**By 1. SOFIA ERNEST VIANGA**
**2. MOSES ERNEST VIANGA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 09th day of **JUNE .........2022**
Dated at MOROGO this 19day of **MAY .........2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**RESIDENT MAGISTRATE**

**RAMASHA COMPANY LIMITED**
**PLOT NO. 212 BLOCK NO. EE, HOUSE NO. 3 NGARENARO,**
**P.O.BOX 1376, ARUSHA- TANZANIA**
**MEMBERS VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY THE COMPANIES**
**ACT, 2002**

Notice is hereby given that the members of **RAMASHA COMPANY LIMITED** have resolved to wind up the company voluntarily and that **Mr. FAISAL SAMSON SALIM RUKAKA of L&L ATTORNEYS AT LAW, P.O.Box 86, Arusha**, Tanzania has been appointed as a liquidator for the purpose of winding up the company.

Creditors of **RAMASHA COMPANY LIMITED** are required on and before 7th July, 2022 to send their names and address with full particulars of their debts or claims against the said company to the liquidator and proof of their debts or claims. Creditors will be excluded from the benefits of any distribution made before such debts are proved.

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Wajumbe chama tawala Nigeria, washiriki kura ya mchujo

**ABUJA,** NIGERIA

WAJUMBE wa chama tawala nchini Nigeria cha All Progressive Congress (APC) wamekutana usiku wa kuamkia jana kushiriki kura ya mchujo ya kumchagua mgombea atakayepeperusha bendera ya chama hicho katika uchaguzi mkuu ujao.

Rais Muhammadu Buhari anafikia ukingoni katika awamu ya pili ya uongozi wake.

Msemaji wa Buhari, Garba Shehu, alisema kiongozi huyo hana mgombea anayempendelea kutoka chama hicho tawala.

Wagombea waliojitokeza kuwania tiketi ya chama hicho ni pamoja na gavana wa zamani wa Lagos, Bola Tinubu, Makamu wa Rais Yemi Osibanjo, waziri wa zamani wa uchukuzi Rotimi Amaechi na kiongozi wa bunge la seneti Ahmad Lawan.

Buhari ambaye kisheria hawezi kugombea tena, anamaliza muhula wake mwaka 2023 baada ya miaka minane, na hivyo kusababisha uvumi juu ya mgombea atakayemuunga mkono kuwa mrithi wake.

Baada ya Buhari ambaye ni muislamu kutoka kaskazini mwa Nigeria kushika hatamu za uongozi, wachambuzi wa kisiasa wanatarajia kuona mgombea wa urais atatokea upande wa kusini kwenye idadi kubwa ya Wakristo kulingana na makubaliano yasiyo rasmi ya marais waislamu na wakristo kupokezana.

Mgombea huyo wa urais kupitia chama tawala alitarajiwa kutangazwa jana japo tangazo hilo limechelewa kutolewa.

## Ubelgiji kurudisha mali zilizoporwa wakati wa ukoloni

**KINSHASA,** DRC

MFALME Phillipe wa Ubelgiji, amesema ataanzisha mpango wa urejeshaji wa mali kale zilizoporwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Akizungumza wakati akianza ziara yake ya wiki moja nchini humo, alisema vitu hivyo viliporwa wakati wa utawala wa babu yake, Mfalme Leopold II.

Mfalme Philippe, na mkewe Malkia Mathilde na wajumbe wa serikali ya Ubelgiji wako katika ziara ya wiki moja nchini humo ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu achukue kiti hicho mwaka 2013.

Miaka miwili iliyopita, alieleza kile alichokiita majuto yake makubwa kwa majeraha ya ukoloni, chini ya Mfalme Leopold.

Mfalme Philippe anatarajiwa kukabidhi kazi ya kwanza kati ya zaidi ya 80,000 zilizoporwa wakati wa ukoloni na kutembelea miji ya kikanda ya Lubumbashi na Bukavu.

**Habari zote na DW**



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Filex Tshisekedi, akisalimiana na Mfalme wa Ubelgiji, Philippe na mkewe Malkia Mathilde alipowasili nchini humo kwa ajili ya ziara ya wiki moja. **PICHA: BBC.**

# Uturuki yaitetea Russia kuondolewa vikwazo

**ANKARA,** UTURUKI

UTURUKI imesema matakwa ya Russia ya kutaka vikwazo dhidi yake kuondolewa ni halali ili kuruhusu usafirishaji wa nafaka kutoka Ukraine.

Mamilioni ya shehena za nafaka zimezuiwa bandarini kufuatia mzingiro wa vikosi vya Russia.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov alikutana na mwenzake wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu, kwa ajili ya kuzungumzia mzozo huo mjini Ankara.

Mazungumzo yao yamejikita zaidi kwenye juhudi za kufungua njia za kusafirisha nafaka za Ukraine hususan ngano ambayo imekwama kwenye bandari zake.

Cavusoglu alisema mpango wa Umoja wa Mataifa kufungua njia kuanza usafirishaji na uuzaji wa nafaka kutoka Ukraine ni wa kuridhisha na unahitaji mazungumzo zaidi wa pande zote husika kuhakikisha meli zitakuwa salama.

Siku ya Jumatatu Rais Zelensky, alisema wana takriban tani milioni 20 na 25 za nafaka ambazo zimezuiwa bandarini. Endapo zitabaki hadi msimu wa vuli, basi tani hizo zinaweza kuongezeka na kufikia milioni 70 hadi 75.

Akizungumza akiwa karibu na Lavrov, Cavusoglu aliongeza kuwa mkutano wao ulikuwa wenye matunda ikiwemo nia ya kurejesha mazungumzo kati ya Russia na Ukraine kuhusu uwezekano wa kusitisha mashambulizi.

"Ikiwa tunahitaji kufungua soko la kimataifa kwa nafaka za Ukraine, alizeti na mafuta yake, basi tunapaswa kuzingatia kuondolewa kwa visiki vilivyoko dhidi ya bidhaa za Russia kama matakwa halali," alisema Cavusoglu.

Kufuatia ombi la Umoja wa Mataifa, Uturuki ilisema itatoa huduma za kuusindikiza msafara wa meli zitakazosafirisha nafaka hizo kutoka bandari za Ukraine.

Athari za vita hivyo vimeendelea kushuhudiwa huku Benki ya Dunia ikipunguza ukuaji wake hadi asilimia 2.9, ikiwa ni asilimia 1.2 chini ya ubashiri wake wa Januari.

Pande zote katika mgogoro huo zinashutumiana kwa kuharibu mashamba ya kilimo, hali inayotishia uhaba zaidi wa chakula ulimwenguni.

Mashambulizi ya Russia katika siku za hivi karibuni nchini Ukraine yamekuwa yakiulenga zaidi mji wa kimkakati wa Severodonetsk.

**RUSSIA YALENGA KUDHIBITI MJI WA SEVERODONETSK**

Katika hotuba yake ya kila siku, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, aliendeleza kutetea ushujaa wa jeshi lake, akisema kwamba ulinzi wa eneo la Donbas unaendelea.

Katika jimbo la Luhansk, miji ya Severodonetsk na Lyschansk ambayo imetengwa na mto, ndiyo pekee ingali chini ya udhibiti wa Ukraine.

Mashambulizi ya Russia katika siku za hivi karibuni nchini humo yamekuwa yakiulenga zaidi mji wa kimkakati wa Severodonetsk.

Hatua hiyo ni baada ya vikosi vya Russia kushindwa na kutimuliwa kutoka maeneo mengine ya nchi.

**RUSSIA YADAI KUDHIBITI JIMBO LA LUHANSK**

Juzi vikosi vya Russia vilikuwa vimechukua udhibiti kamili wa maeneo kadhaa ya makazi ya watu, huku vikosi vya Ukraine vikidhibiti maeneo ya viwanda na viunga vyake.

Hata hivyo maofisa wa Ukraine wamekanusha kwa msisitizo mkubwa kuwa majeshi ya Russia hayaudhibiti mji huo.

Gavana wa jimbo la Luhansk, Sergiy Gaiday amesema huenda alisema vikosi vya Ukraine vikalazimika kurudi nyuma.

Akihojiwa na kituo cha televisheni cha Channel 1+1 nchini humo, alisema inawezekana watarudi nyuma katika maeneo yenye ulinzi zaidi.

Baada ya vikosi vya Russia kutimuliwa maeneo ya Kyiv na maeneo mengine, vikosi vyake sasa vimeimarisha mashambulizi kulenga maeneo ya Donbas yaliyoko majimbo ya Luhansk na Donetsk.

**MERKEL ATETEA UHUSIANO WAKE NA RUSSIA**

Kansela aliyeondoka wa Ujerumani Angela Merkel, ametetea sera yake ya kudumisha uhusiano na Russia wakati alipokuwa madarakani.

Alisema anaona hakuna lolote la kuomba msamaha licha ya kuibuka mzozo wa Ukraine na kuonekana kuutia doa uongozi wake.

Katika mahojiano yake ya kwanza tangu alipoondoka madarakani miezi sita iliyopita, Merkel alisema hakuwa mjinga katika kuelewana na Rais wa Russia Vladimir Putin.

Merkel mwenye umri wa miaka 67, ameeleza katika mahojiano hayo yaliyopeperushwa kupitia chaneli ya habari ya Phoenix, kuwa diplomasia sio jambo baya kwa sababu tu haikufanya kazi. Kansela huyo wa zamani pia aligusia jinsi alivyounga mkono vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Russia baada ya nchi hiyo kulitwaa kwa nguvu eneo la Crimea mwaka 2014 pamoja na juhudi za Ujerumani na Ufaransa za kuuweka hai mkataba wa amani wa Minsk, ambao ulikuwa ni makubaliano ya kusitisha mapigano mashariki mwa Ukraine.

Kiongozi huyo ambaye mara kwa mara alikutana na Putin wakati wa mihula yake minne, alisema hakuna sababu yoyote ya kuhalalisha vita nchini Ukraine na kwamba Putin amefanya kosa kubwa.

HABARI MICHEZO

# KHALID SASA KURITHI MIKOBA YA VIVIER BIASHARA UNITED

**Na Saada Akida**

KOCHA wa zamani wa Mwadui FC, Khalid Adam, anatarajiwa kupewa mikoba ya kukinoa kikosi cha Biashara United, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha timu hiyo haishuki daraja.

Biashara United ambayo mapema wiki hii ilivunja benchi lake la ufundi kwa kuwaondoa Kocha Mkuu, Vivier Bahati, msaidizi wake pamoja na meneja wa timu hiyo, inashika nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na pointi 24 sawa na Mbeya Kwanza inayoburuza mkia kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka ndani ya timu hiyo, zimeeleza kuwa uongozi umeridhia kumpa mikoba hiyo Khalid ili kukiongoza kikosi hicho hadi mwishoni mwa msimu. Kilisema Khalid ataendelea na majukumu ya kuinoa na kusimamia timu hiyo kuhakikisha anaisaidia kupambana kupata matokeo mazuri katika michezo iliyosalia ili kuinusuru kushuka daraja.

"Ni kweli tuko katika mazungumzo na Khalid na matarajio yetu makubwa ni kuona anasaidia timu kupata matokeo mazuri katika mechi tulizobakiza ili kuinusuru kushuka daraja," alisema mtoa habari huyo.

Hata hivyo, Nipashe lilipomtafuta Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, hakutaka kuweka wazi juu ya kocha huyo zaidi ya kudai kwamba wako katika mchakato wa kutafuta mtu ambaye ataendelea walipoishia na kuinasua katika nafasi ya kushuka daraja.

"Hatuwezi kwenda katika michezo iliyosalia bila ya kuwa na kocha, tuko katika mchakato na muda wowote tutaweka wazi nani anachukua nafasi ya kocha mkuu," alisema Mataso.

TULIA KWANZA...



Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, akitoa maelekezo kwa kiungo wa timu hiyo, Sadio Kanouté, wakati wa mazoezi yaliyofanyika katika Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam juzi. **PICHA: SIMBA**

# Dodoma Jiji yamuundia 'tume' Mpole

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji, imesema itakwenda kwa tahadhari zote kucheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold Juni 13 kwenye Uwanja wa Nyamkumbu, Geita, lakini ikimwekea mikakati straika George Mpole asiweze kuleta madhara.

Kocha wa makipa wa timu hiyo, Adam Moshi, amesema anawaandaa makipa wake kwa ajili ya kukabiliana na michomo ya wachezaji wa Geita Gold, lakini hasa Mpole ambaye kwa sasa ameibukia kuwa straika hatari nchini.

"Kazi yangu mimi hapa ni kuwapa mbinu makipa wangu ili kukabiliana na hatari na mashuti ya wachezaji wa Geita Gold, kwa sasa wana mtu anaitwa Mpole, nafanya kazi kubwa ya kuwaelekeza ili wawe makini naye," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Masoud Djuma, yeye amesema watakwenda kucheza na timu nzuri, bora na yenye matokeo mazuri kuliko wao, lakini ni ngumu kufungika kwao, hivyo itabidi wafanye kazi ya ziada.

"Ni timu nzuri, ina kocha mzuri, wako kwenye nafasi nzuri, nasikia pia ina wachezaji wazuri, sijawahi kuwaona na mimi kama kocha itakuwa ni mara yangu ya kwanza kucheza nao, nasikia pia hawafungiki wakicheza kwenye uwanja wao, lakini tutajipanga kwenda kucheza na mpinzani ambaye yuko vizuri," alisema kocha huyo.

Dodoma Jiji ipo kwenye nafasi ya 11 ikiwa na pointi 36, ikibakisha mechi nne, huku Geita Gold ikiwa nafasi ya tano ikikusanya alama 36 katika msimamo wa ligi hiyo.

# Mfaume ampania bondia Mmisri Julai

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Mfaume Mfaume amesema atahakikisha anaendelea kujiandaa vizuri kuelekea pambano lake la Julai Mosi, mwaka huu dhidi ya Mmisri Abdumonem Said, ili kurejea katika orodha ya mabondia wa kimataifa.

Mfaume aliondolewa katika orodha hiyo baada ya kutopanda jukwaani kwa muda wa mwaka mmoja na nusu na sasa atapanda tena ulingoni Julai Mosi, mwaka huu, dhidi ya bondia huyo kutoka Misri, Abdumonem kwenye pambano la ubingwa wa Mkanda wa WBF.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mfaume alisema amejiandaa vya kutosha na atafanya vizuri katika pambano hilo ili kuhakikisha anabakiza mkanda huo nchini na kurejea katika orodha ya mabondia wa kimataifa.

Alisema kwa sasa anaendelea na maandalizi yake ili kujiandaa kikamilifu chini ya Kocha wake, Rama Jah, lengo likiwa ni kufanya vizuri katika pambano hilo ambalo anaamini litamrejesha katika ramani ya masumbwi kimataifa.

"Nimejiandaa vizuri dhidi ya Abdumonem, ni bondia mzuri, nimemfuatilia na nimeona ubora wake, nimejiandaa vizuri kukabiliana na mpinzani wangu huyo na kuhakikisha naipeperusha vema bendera ya Tanzania, nitahakikisha nampiga huyo Mmisri hapa nyumbani," alisema Mfaume.

Alisema amepata muda wa kutosha kujiandaa na kufanikiwa kufanyia kazi mbinu za mpinzani wake huyo, hivyo anaamini atakuwa bora zaidi na kuleta heshima kwa taifa.



## ZISIKUPITE

### CITY YAMKANA SAKA
KLABU ya Manchester City imekataa taarifa kwamba, inajiandaa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na England, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

### TCHOUAMENI KUTUA MADRID
REAL Madrid wamekubaliana mkataba wenye thamani ya euro milioni 100 na Monaco kwa ajili ya kiungo wa kati Mfaransa, Aurelien Tchouameni. ***(Athletic)***

### RASHFORD ANUKIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo na mshambuliaji wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24, kwa ajili ya kuhamia katika klabu hiyo ya Kaskazini mwa London. ***(Caught Offside)***

### BOTMAN AKARIBIA MILAN
AC Milan wana matumaini ya kukamilisha kumsajili mlinzi Uholanzi, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22, na kiungo wa kati wa Ureno, Renato Sanches mwenye miaka 24, kutoka Lille. ***(90min)***

### NUNEZ AGOMBEWA EPL
KLABU ya Manchester United na Newcastle kwa pamoja zinaripotiwa kuwa kwenye mbio moja kumuwania kumsajili, mshambuliaji wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22. ***(Sebastian Giovanelli via Star)***

### TUCHEL AAHIDIWA CHELSEA
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel ameahidiwa na mmiliki wa klabu hiyo, Todd Boehly kuwa anaweza kuongoza kazi ya usajili ili kuimarisha kikosi kipya. ***(Telegraph)***

### BISSOUMA HATAKIWI VILLA
KIUNGO wa kati wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25, hayuko tena katika orodha ya wachezaji wanaopangwa kuchukuliwa na Aston Villa. Hata hivyo, kocha wa Villa, Steven Gerrard anaweza kuendelea kumtafuta kiungo wa kati msimu huu. ***(Athletic)***

### LEWANDOWSKI NA BAYERN
MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, alikiambia kipindi cha matangazo ya mtandaoni (podcast) kwamba anaondoka Bayern Munich kwa sababu anataka "hisia zaidi" katika maisha yake na mabingwa hao wa Ujerumani "hawakutaka kunisikiliza hadi mwisho". ***(Bild)***

### ERIKSEN AWINDWA WEST HAM
KLABU ya West Ham imetuma kikosi cha kumfuatilia kiungo wa kati wa Denmark na Brentford, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30. ***(Star)***

### ADAM ATAKIWA LEEDS
KLABU ya Leeds United imejiunga na Southampton pamoja na West Ham katika nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Austria, Junior Adamu mwenye umri wa miaka 20. (Sky Sports Austria)

### VAN PERSIE ALIMGOMEA TEN HAG
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Uholanzi, Robin van Persie mwenye umri wa miaka 38, amesema kuwa alikataa fursa ya kujiunga na Erik ten Hag kama kocha msaidizi hapo Old Trafford. ***(Mirror)***

### DE JONG NA UNITED
BARCELONA wako tayari kwa mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, kuelekea Old Trafford, lakini klabu hiyo ya Hispania bado haijapokea ofa rasmi kutoka United. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI: SITALAZIMISHA KWENDA KUJIUNGA NA BARCA

●●●Nadhani ni bora kwa Bayern kuwekeza fedha wanazoweza kupata nikiuzwa kuliko kuniweka hadi...

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski haoni uadui wowote dhidi ya Bayern Munich na hatalazimisha kuondoka, lakini amesisitiza kumruhusu kuondoka litakuwa jambo la manufaa kwa pande zote mbili.

Barcelona wamekuwa wakihusishwa na kutaka kumsajili Lewandowski ambaye anataka kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, badala ya kuongeza mkataba unaotarajiwa kumalizika mwakani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland wiki hii alisema "kitu kimekufa" ndani yake, na kwamba anataka kuondoka Bayern "kupitia hisia mpya."

Bayern wamebaki na msimamo kwamba, Lewandowski lazima amaliza mkataba wake, huku ripoti zikisema Barca inaweza kuwa na ugumu wa kukamilisha uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33.

Lewandowski amesisitiza kuwa wababe hao wa Bavaria watakuwa wamefanya jambo bora zaidi kama wakimruhusu aondoke.

"Nadhani ni bora kwa Bayern kuwekeza fedha wanazoweza kupata nikiuzwa kuliko kuniweka hadi mwisho wa mkataba," alisema Lewandowski akiliambia gazeti la Bild.

"Sitaki kulazimisha chochote, hiyo si maana. Natafuta suluhisho bora.

"Nataka imalizike: hisia lazima zipoe. Nataka kuzungumza kwa utulivu, si kupitia vyombo vya habari. Najua kwamba mzozo unazua vichwa vingi vya habari. Lakini FC Bayern na mimi si maadui."

Aliongeza: "Sina ubinafsi. Ninajua nilichokuwa nacho Bayern na ninakithamini sana. Pia najua kwamba nimekuwa nikifanya kila niwezalo kutowakatisha tamaa, nimekaa kwa miaka nane."

Lewandowski aliifungia Bayern mabao 35 kwenye Bundesliga msimu wa 2021-22, na kunyakua Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya kwa mwaka wa pili mfululizo.

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,004,0

MECHI KALI

PORTUGAL

VERSUS

CZECH REPUBLIC

1 | 1.43
X | 4.53
2 | 6.65

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ


PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SAKA HANA HARAKA NA MKATABA ARSENAL



**LONDON, England**

BUKAYO Saka hana haraka ya kuongeza mkataba wake Arsenal, licha ya 'Washikabunduki' hao kutaka kuanzisha mazungumzo msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa 90min.

Saka alikuwa na kiwango cha kuvutia msimu uliopita, na kuibuka kuwa mchezaji nyota wa timu hiyo ya Kaskazini mwa London huku akipachika mabao 11 na kutoa asisti saba katika mechi 38 za Ligi Kuu England.

Mshambuliaji huyo chipukizi alitia saini mkataba wake wa sasa mwaka 2020 baada ya msimu wake kuimarika, lakini Arsenal wanafahamu vema kwamba anastahili kuboreshewa mkataba.

Na 90min imethibitisha kwamba 'Washikabundu' hao wanataka kumpa mkataba mpya Saka ambaye amekuwa akiwaniwa na timu kadhaa.

Saka anakaribia kuingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake pale Emirates, lakini Arsenal wana fursa ya kuongeza mkataba na tayari wamemwambia mchezaji huyo wanapanga kuanzisha mazungumzo.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, hafikirii kuwa katika haraka yoyote ya kuongeza mkataba mpya, huku timu kadhaa zikimfuatilia kwa makini.

Manchester City na Liverpool zote zimetajwa kuwa na mpango wa kuwania saini ya Saka.


# Guardiola aitabiria makubwa Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema Barcelona watarudi katika ubora wao ndani ya "mwaka mmoja au miwili."

Barcelona imekumbwa na matatizo ya kifedha ndani na nje ya uwanja katika miaka ya hivi karibuni, lakini walipiga hatua nzuri msimu uliopita kwani kocha mpya, Xavi aliiongoza kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, lakini wakiwa nyuma kwa pointi 13 dhidi ya mabingwa, Real Madrid.

Guardiola, ambaye alikiri Xavi amefanya "kazi nzuri" katika muda wake mfupi hapo Camp Nou, aliwataka mashabiki kubaki na subira huku Barca wakiendelea kujiimarisha na kutabiri matokeo chanya katika siku



za usoni.

"Siku zote ni ngumu wakati huwezi kufanya mambo makubwa, lakini lazima uwe mtulivu," alisema Guardiola akinukuliwa na AS.

"Kuna wakati katika historia inabidi ukubali kwamba hali ndivyo ilivyo. Wakati mwingine.

"Hali ya uchumi ndivyo ilivyo, sizungumzii ubora wa makocha, mameneja au wachezaji, fikra nilizonazo ni kwamba wote ni wazuri, lakini wakati mwingine ni lazima uwe mtulivu kwa mwaka mmoja au miwili na haitakuwa rahisi bila kuweza kufanya usajili mzuri.

"Sasa hali ndivyo ilivyo, wanapaswa kujikubali wao ni nani na kujaribu tu kushinda mchezo unaofuata na unaofuata. Lakini ukubali kwamba hali ndivyo ilivyo."

HABARI MICHEZO

055,092/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.11/06/22 | 19:00 | Faroe Islands vs Lithuania | 2.31 | 2.90 | 3.30 |
| 02.11/06/22 | 19:00 | Ireland vs Scotland | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 03.11/06/22 | 21:30 | Arsenal Sarandi vs Banfield | 2.70 | 3.05 | 2.65 |
| 04.11/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Bosnia and Herzegovina | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 05.11/06/22 | 22:00 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 3.05 | 3.35 | 2.20 |
| 06.11/06/22 | 22:00 | Girona vs Tenerife | 2.32 | 3.10 | 3.05 |
| 07.12/06/22 | 00:00 | Sarmiento vs Argentinos Juniors | 3.05 | 3.15 | 2.28 |
| 08.12/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Bragantino SP | 2.80 | 3.05 | 2.55 |
| 09.13/06/22 | 01:00 | Tombense MG vs CSA AL | 2.70 | 2.75 | 2.90 |
| 10.12/06/22 | 03:00 | Internacional vs Flamengo | 2.80 | 3.30 | 2.37 |
| 11.12/06/22 | 07:00 | Renofa Yamaguchi vs Fagiano Okayama | 3.05 | 2.95 | 2.44 |
| 12.12/06/22 | 08:00 | Mito Hollyhock vs Montedio Yamagata | 2.60 | 3.10 | 2.65 |
| 13.12/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Omiya Ardija | 2.41 | 3.00 | 3.05 |
| 14.12/06/22 | 19:00 | Colon Santa Fe vs Union Santa Fe | 2.43 | 2.95 | 3.05 |
| 15.12/06/22 | 21:30 | Godoy Cruz vs Racing Club | 2.47 | 3.25 | 2.75 |
| 16.12/06/22 | 22:00 | Vasco da Gama vs Cruzeiro | 2.65 | 2.90 | 2.80 |
| 17.12/06/22 | 22:00 | Sporting Kansas City vs New England Revolution | 2.85 | 3.40 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 09/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1758 | Tianjin Teda vs Shenzhen | 4.61 | 3.58 | 1.66 |
| 15:00 | 2070 | Boca Jrs vs CA Central Cordoba SE Reserve | 1.48 | 4.02 | 5.69 |
| 15:00 | 3790 | San Lorenzo de Almagro Res. vs Newells Old Boys | 2.61 | 3.25 | 2.45 |
| 15:30 | 4776 | Venezuela Youth vs Colombia Youth | 2.80 | 3.19 | 2.33 |
| 16:00 | 2557 | South Sudan vs Mali | 10.13 | 4.86 | 1.31 |
| 16:00 | 2795 | Saudi Arabia U23 vs United Arab Emirates U23 | 1.63 | 3.44 | 5.11 |
| 16:00 | 4739 | Japan U23 vs Tajikistan U23 | 1.09 | 7.26 | 22.57 |
| 16:00 | 5812 | Burundi vs Cameroon | 9.90 | 4.34 | 1.35 |
| 17:00 | 1739 | Atletico Tucuman Reserve vs CA River Plate (Arg) | 3.05 | 3.25 | 2.15 |
| 17:00 | 3173 | CA Talleres de Cordoba Reserve vs Independiente Reserve | 2.25 | 2.95 | 3.15 |
| 19:00 | 1161 | Musa Pori vs EPS | 1.44 | 4.40 | 5.67 |
| 19:00 | 1575 | PPJ vs KuPS Akatemia | 1.56 | 4.12 | 4.61 |
| 19:00 | 1581 | Sweden U21 vs Italy U21 | 2.76 | 3.45 | 2.24 |
| 19:00 | 4029 | Nigeria vs Sierra Leone | 1.29 | 5.25 | 9.49 |
| 19:00 | 4187 | Guinea vs Malawi | 1.38 | 4.44 | 8.27 |
| 19:00 | 4795 | AIK W vs Pitea W | 4.42 | 3.78 | 1.64 |
| 19:00 | 4869 | France U18 vs Mexico U22 | 1.60 | 3.68 | 4.91 |
| 19:00 | 5880 | Slovenia U21 vs Andorra U21 | 1.04 | 9.22 | 34.31 |
| 19:45 | 4807 | Ukraine U21 vs France U21 | 3.34 | 3.54 | 1.93 |
| 20:00 | 1848 | Lindome Gif vs Qviding Fif | 2.31 | 3.44 | 2.65 |
| 20:00 | 2018 | Hassleholms IF vs Osterlen FF | 1.96 | 3.73 | 3.09 |
| 20:00 | 2031 | Saudi Arabia vs Venezuela | 3.26 | 3.00 | 2.38 |
| 20:00 | 4844 | IF Algarna vs Sund IF | 1.79 | 3.49 | 3.93 |
| 20:00 | 5178 | Lesotho vs Ivory Coast | 8.27 | 4.54 | 1.37 |
| 20:30 | 3940 | Landvetter IS vs BK Astrio | 2.61 | 4.03 | 2.13 |
| 21:45 | 2550 | Sweden vs Serbia | 2.57 | 3.12 | 2.77 |
| 21:45 | 2957 | Norway vs Slovenia | 1.43 | 4.25 | 7.49 |
| 21:45 | 3740 | North Macedonia vs Georgia | 2.22 | 3.03 | 3.44 |
| 21:45 | 3976 | Switzerland vs Spain | 3.93 | 3.43 | 1.91 |
| 21:45 | 4066 | Gibraltar vs Bulgaria | 13.10 | 6.25 | 1.20 |
| 21:45 | 4104 | Portugal vs Czech Republic | 1.43 | 4.53 | 6.65 |
| 21:45 | 5894 | Malta vs Estonia | 2.52 | 3.07 | 2.87 |
| 21:45 | 5918 | Kosovo vs Northern Ireland | 2.13 | 3.14 | 3.54 |
| 21:45 | 5969 | Greece vs Cyprus | 1.23 | 5.43 | 14.08 |
| 22:00 | 2279 | Morocco vs South Africa | 1.54 | 3.79 | 6.46 |
| 22:00 | 3108 | Dominica vs Saint Lucia | 2.46 | 3.10 | 2.70 |
| 22:15 | 1769 | HK Kopavogur W vs FH Hafnarfjordur W | 5.88 | 5.10 | 1.36 |
| 22:15 | 2076 | IR Reykjavik vs Reynir Sandgerdi | 1.38 | 5.11 | 5.50 |
| 22:15 | 2136 | UMF Selfoss vs Fylkir | 3.88 | 3.93 | 1.70 |
| 22:15 | 2278 | KV Vesturbaer vs Afturelding | 2.55 | 3.63 | 2.31 |
| 22:15 | 3838 | Haukar W vs Vikingur Reykjavik W | 6.46 | 5.29 | 1.32 |
| 22:15 | 5689 | UMF Grindavik vs Fjolnir | 2.56 | 3.59 | 2.32 |
| 22:15 | 5875 | Njarovik vs Haukar | 1.51 | 4.61 | 4.51 |
| 22:45 | 4305 | KF Fjallabyggd vs Magni | 2.34 | 3.77 | 2.45 |

IJUMAA - 10/06/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 4381 | Palmeiras vs Botafogo RJ | 1.41 | 4.12 | 6.67 |
| 02:00 | 1708 | Fortaleza CE vs Goias | 1.54 | 3.54 | 5.90 |
| 02:00 | 4846 | Coritiba vs Sao Paulo | 3.14 | 2.94 | 2.27 |
| 03:00 | 3332 | Panama vs Martinique | 1.12 | 6.87 | 16.67 |
| 05:30 | 2494 | Canada vs Curacao | 1.15 | 6.10 | 14.76 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MCHENGERWA ATOA RAI TEMBO WARRIORS POLAND

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, ameitaka timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu, Tembo Warriors, kuhakikisha inaendeleza kasi yake ya kufanya vizuri kwenye michuano ya Ulaya inayokwenda kushiriki nchini Poland.

Mchengerwa alitoa raia hiyo jana wakati akiiaga na kuikabidhi Bendera ya Taifa, kuelekea mjini Warsaw, Poland kushiriki michuano ya Ulaya ambayo wataitumia kama sehemu ya maandalizi ya Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Uturuki.

Mchengerwa alisema: "Nendeni mkatumie vizuri mbinu pamoja na maelekezo ambayo mmepewa na walimu wenu, naamini mtafanya vizuri kwani tayari mmeifungulia njia Tanzania kushiriki Kombe la Dunia."

Alisema serikali itaongeza nguvu kwenye michezo yote inayofanya vizuri ikiwa ni agizo ambalo lilitolewa juzi na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Akson.

"Sisi kama serikali tutakuwa bega kwa bega na viongozi wenu kwani wametuheshimisha, hatuna jambo dogo rais wetu anataka ushindi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Soka nchini, Yusuph Singo, alisema timu hiyo imefanya maandalizi ya muda mrefu ikiwamo kukaa kambini tangu Februari 20, mwaka huu mpaka jana ilipoanza safari kuelekea nchini Poland kwa michuano hiyo ambayo itashiriki kama timu alikwa.

Alisema timu ambazo watakutana nazo ndizo ambazo zitakwenda kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia, hivyo watajifunza mambo mengi ambayo yatawasaidia kufanya vizuri.

NIMEZIPIGA...




Mshindi wa Bonasi ya Supa Jackpot, Thomas Lumbillah Mhanga, akionyesha mfano wa hundi ya shilingi 12,704,063 baada ya kukabidhiwa kutokana na kubashiri kwa usahihi mechi 14 kati ya 17 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

# Kipanga waifuata Chipukizi fainali FA Cup

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kipanga imeifuata Chipukizi ya Pemba Fainali ya Michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, baada ya kuwafunga Maafande wenzao wa Mafunzo kwa mabao 2-0 katika mchezo wa nusu fainali ya pili Kanda ya Unguja.

Mabao ya Kipanga katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Amaan juzi, yalifungwa na Mundhiri Abdallah dakika ya tatu na Abdallah Iddi dakika ya 42 .

Kwa matokeo hayo sasa Kipanga itakuwa na shughuli pevu katika mchezo dhidi ya Chipukizi kutoka Kisiwani Pemba baadaye mwezi huu katika Uwanja wa Amaan. Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Kipanga, Khamis Hassan, alianza kwa kuwapongeza wachezaji wake kwa kuhakikisha wanafanikiwa kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo.

Alisema baada ya kutinga fainali, sasa wanaendelea na maandalizi ya mchezo huo ili kuhakikisha wanafanya vizuri.

Alisema lengo lao kubwa ni kuhakikisha wanachukua ubingwa huo, hivyo lazima wafanye maandalizi mazuri.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Ali Bakari, tarehe ya mchezo wa fainali ya haijapangwa, lakini kuhusu uwanja itakuwa katika Dimba Amaan.

Alisema kama ilivyotangazwa hapo awali, bingwa wa michuano hiyo atajinyakulia kitita cha Shilingi milioni 30 kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ambao ni wadhamini wakuu wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.